# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA KILIMO
# BODI YA KOROSHO TANZANIA



**KABRASHA LA KIKAO CHA TATHMINI YA UZALISHAJI, UBANGUAJI NA MASOKO YA KOROSHO MSIMU WA 2024/2025 NA MIPANGO YA MSIMU WA 2025/2026**

**TAREHE 30 APRILI, 2025**

**KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA PSSSF – JIJINI DODOMA**

**APRILI, 2025**

## AGENDA NA. 1: KUFUNGUA KIKAO

**AGENDA NA. 2: KUTHIBITISHA AGENDA**

**AGENDA ZA KIKAO CHA TATHMINI YA UZALISHAJI, UBANGUAJI NA MASOKO YA KOROSHO MSIMU WA 2024/2025 NA MIPANGO YA MSIMU WA 2025/2026 TAREHE 30 APRILI, 2025 KATIKA UKUMBI WA PSSSF JIJINI DODOMA**

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Kupitia Muhtasari wa kikao cha tathmini ya uzalishaji, Ubanguaji na masoko ya korosho kilichofanyika tarehe 22 Aprili, 2024.
4. Kupitia utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha tathmini ya uzalishaji, ubanguaji na masoko ya korosho kilichofanyika tarehe 22 Aprili, 2024.
5. Kupokea taarifa ya tathmini ya uzalishaji, ubanguaji na masoko ya korosho msimu wa 2024/2025 na mipango ya msimu wa 2025/2026:
    a. Uzalishaji,
    b. Masoko, na
    c. Ubanguaji.
6. Taarifa ya maendeleo ya utafiti katika zao la korosho kutoka TARI Naliendele.
7. Taarifa kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) - Mtwara.
8. Taarifa kutoka Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi ya Ghala (WRRB).
9. Taarifa kutoka Soko la Bidhaa Tanzania (TMX)
10. Taarifa kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC).
11. Mengineyo.
12. Kufunga kikao.

**AGENDA NA. 3: KUPITIA MUHTASARI WA KIKAO CHA TATHMINI YA UZALISHAJI, UBANGUAJI NA MASOKO YA KOROSHO KILICHOFANYIKA TAREHE 22 APRILI, 2024**

**MUHTASARI WA KIKAO CHA TATHMINI YA UZALISHAJI, UBANGUAJI NA MASOKO YA KOROSHO MSIMU WA 2023/2024 NA MIPANGO YA MSIMU WA 2024/2025 KILICHOFANYIKA TAREHE 22 APRILI, 2024 KATIKA UKUMBI WA PSSSF - JIJINI DODOMA**

**MAHUDHURIO**

1. Mhe. Hussein M. Bashe (Mb) - Waziri wa Kilimo
2. Mhe. George H. Mkuchika - Waziri Ofisi ya Rais
3. Ndg. Gerald Mweli *ndc* - Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo
4. Dkt. Hussein Omar - Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo
5. Ndg. Yusuph S. Nanila - Mwenyekiti wa Mkutano wa Wadau

**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**

6. Mhe Deodatus Mwanyika - Mwenyekiti
7. Mhe. Salma R. Kikwete - Mbunge
8. Mhe Mariam M. Ditopile - Mbunge
9. Mhe Janejelly James Ntale - Mbunge
10. Mhe Yustina Rahi - Mbunge
11. Mhe Francis Isack Mtinga - Mbunge
12. Mhe Prof. Patrick Ndakidemi - Mbunge
13. Mhe. Pauline Gekul - Mbunge
14. Mhe. Kunti Majala - Mbunge
15. Mhe. Dkt. Christine Ishengoma - Mbunge
16. Mhe. Dkt. Medard Kalemani - Mbunge
17. Mhe. Ng'wasi Kamani - Mbunge
18. Mhe. Khadija Hassan - Mbunge
19. Mhe. Elizabeth Ngeloma - Mbunge
20. Mhe. Lucy John Sabu - Mbunge
21. Mhe. Antipas Mgungusi - Mbunge
22. Mhe. Tauhida Gallos - Mbunge
23. Mhe. Prof. Sospeter Mohongo - Mbunge

**WABUNGE**

24. Mhe. Shamsia A. Mtamba - Mbunge Jimbo la Mtwara vijijini
25. Mhe. Geofrey L. Mwambe - Mbunge Jimbo la Masasi Mjini
26. Mhe. Dr. Amandus J. Chinguile - Mbunge Jimbo la Nachingwea
27. Mhe. Hassan Z. Kungu - Mbunge Jimbo la Tunduru Kaskazini

28. Mhe. Agnes Hokororo - Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Mtwara
29. Mhe. Subira H. Mgalu - Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Pwani
30. Mhe. Maimuna A. Pathan - Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Lindi
31. Mhe. Mariam N. Kisangi - Mbunge Viti Maalum Dar es Salaam
32. Mhe. Daimu Iddi Mpakate - Mbunge Jimbo la Tunduru Kusini
33. Mhe. Francis K. Ndulane - Mbunge Jimbo la Kilwa Kaskazini
34. Mhe. Tecla Ungele - Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Lindi
35. Mhe. Katani A. Katani - Mbunge Jimbo la Tandahimba
36. Mhe. Twaha Mpembenwe - Mbunge Jimbo la Kibiti
37. Mhe. Mwambe Cecil - Mbunge Jimbo la Ndanda
38. Mhe. Michael Mwakamo - Mbunge Jimbo la Kibaha
39. Mhe. Ally M. Kassinge - Mbunge Jimbo la Kilwa Kusini
40. Mhe. Hassan Mtenga - Mbunge Jimbo la Mtwara Mjini
41. Mhe. Riziki Saidi Lulida - Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Lindi
42. Mhe. Hamida M. Abdallah - Mbunge Jimbo la Lindi
43. Mhe. Muharami S. Mkenge - Mbunge Jimbo la Bagamoyo
44. Mhe. Tunza Issa Malapo - Mbunge Viti Maalum Mtwara
45. Mhe. Maimuna S. Mtanda - Mbunge Jimbo la Newala
46. Mhe. Zuberi Kuchauka - Mbunge Jimbo la Liwale
47. Mhe. Abdallah Chikota - Mbunge Jimbo la Nanyamba
48. Mhe. Mariam Nyoka - Mbunge Viti Maalum Ruvuma
49. Mhe. Anastazia J. Wambura - Mbunge Viti Maalum Mtwara
50. Mhe. Mohamed S. Issa - Mbunge Jimbo la Konde
51. Mhe. Aleksia A. Kamguna - Mbunge Viti Maalum
52. Mhe. Sophia Mwakagenda - Mbunge Viti Maalum
53. Mhe. Maryam A. Mwinyi - Mbunge Viti Maalum Chakechake
54. Mhe. Rehema Migilla - Mbunge Viti Maalum Ulyankulu
55. Mhe. Dr. Thea Ntara - Mbunge Viti Maalum
56. Mhe. Yahaya Massare - Mbunge Jimbo la Manyoni Magharibi
57. Mhe. Mariam N. Kisangi - Mbunge Viti Maalum
58. Mhe. Janeth Mahawanga - Mbunge Viti Maalum
59. Mhe. Benaya Kapinga - Mbunge Jimbo la Mbinga Vijijini
60. Mhe. Jacquline Kainja - Mbunge Viti Maalum
61. Mhe. Agnesta Kaiza - Mbunge Viti Maalum

62. Mhe. Mariam S. Lulipa - Mbunge Viti Maalum

**VIONGOZI WA CCM WA MIKOA**

63. Ndg. Adam Kimbisa - Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma
64. Ndg. Said Nyegedi - Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mtwara
65. Ndg. Martha Mlata - Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida
66. Ndg. Patrick Mwalunenge - Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya
67. Ndg. Hassan Jarufu - Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Lindi
68. Ndg. Benard Elias - Katibu wa CCM Mkoa wa Lindi
69. Ndg. Seleman Sankwa - Katibu wa CCM Mkoa wa Tanga
70. Ndg. Lucy Shee - Katibu wa CCM Mkoa wa Singida
71. Ndg, Mwinshehe Mlao - Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga
72. Ndg. Pili Mbanga - Katibu wa CCM Mkoa wa Dodoma
73. Ndg. Omar Ayoub - Mwakilishi wa CCM Mkoa wa Tanga
74. Ndg. Juma Nakoveka - Katibu wa CCM Mkoa wa Mtwara
75. Ndg. Patrick Magarinja - Katibu wa CCM Mkoa wa Lindi

**WAKURUGENZI BODI YA KOROSHO TANZANIA**

76. Brig. Gen. (Mstaafu) Aloyce D. Mwanjile ndc-Mwenyekiti Bodi ya Wakurugenzi
77. Ndg. Kate Kamba M/Mwenyekiti Bodi ya Wakurugenzi
78. Ndg. Yahya Chomboko - Mjumbe Bodi ya Wakurugenzi
79. Dkt. Fortunus Kapinga - Mjumbe Bodi ya Wakurugenzi
80. Ndg. Rashid M. Hamis - Mjumbe Bodi ya Wakurugenzi
81. Ndg. Faith M. Mitambo - Mjumbe Bodi ya Wakurugenzi
82. Ndg. Musa A. Manjaule - Mjumbe Bodi ya Wakurugenzi
83. Prof. Peter A. Masawe - Mjumbe Bodi ya Wakurugenzi

**TUME MAALUM YA MAPITIO YA TASNIA YA KOROSHO**

84. Ndg. Julius Chacha - Mwenyekiti wa Kamati
85. Ndg. Samson Poneja - Katibu
86. Ndg. Miraji Kapanda - Mjumbe
87. Ndg. Daud Suleiman - Mjumbe
88. Ndg. Debora M. Masengo - Mjumbe
89. Ndg. Bathromeo Ngela - Mjumbe
90. Ndg. Costantine Msoka - Mjumbe

91. Ndg. Generose Ngalawa - Sekretarieti

**SEKRETARIETI ZA MIKOA**

92. Ndg. Emigidius Kasunzu - Katibu Tawala Msaidizi Tanga
93. Ndg. Deogratius Sibula - Katibu Tawala Msaidizi Ruvuma
94. Ndg. Marjid A. Myao - Katibu Tawala Msaidizi Lindi
95. Ndg. Stanslaus B. Choaji - Katibu Tawala Msaidizi Singida
96. Ndg. Shangwe Twamala - Katibu Tawala Msaidizi Pwani
97. Ndg. Aziza R. Mumba - Katibu Tawala Msaidizi Dodoma
98. Dkt. Rozalia Rwegasira - Katibu Tawala Msaidizi Morogoro

**WADAU WA MAENDELEO**

99. Ndg. Reginald Mpolo - Mkurugenzi wa Mipango Care Tanzania
100. Ndg. Allen Kaijanangoma - Afisa CARE Tanzania
101. Ndg. Christopher Mazali - Meneja CARE Tanzania
102. Ndg. Edith Razaro - Afisa ASPIRES

**WIZARA NA TAASISI MBALIMBALI**

103. Dkt. Benson Ndiege - Mrajis wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika
104. Ndg. Asangye Bangu - Mkurugenzi Mtendaji WRRB
105. Ndg. Patrick M. Mongella - Mkurugenzi Mkuu CPB
106. Ndg. Nyatega Michael - Katibu Ikulu
107. Ndg.Godfrey Malekamo - Afisa Mtendaji Mkuu TMX
108. Ndg. Nyasebwa Chimangu - Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo
109. Ndg. Tagie Mwakawago - Mkurugenzi wa Mawasiliano Wizara ya Kilimo
110. Ndg. Upendo Mndeme - Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Ugani Wizara ya Kilimo
111. Ndg. Obadia Nyagiro - Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Kilimo
112. Ndg. George Bokki - Afisa Kilimo Wizara ya Kilimo
113. Ndg. Matondo Matondo - Katbu wa Naibu Waziri Kilimo

114. Ndg. James Kyejo - Katibu wa Waziri wa Kilimo
115. Ndg. Lilanga Mohamed J - Afisa TCDC
116. Ndg. Robert Nsunza - DCO TCDC
117. Ndg. Cesilia Sostenes - Mrajis Msaidizi Lindi
118. Ndg. Abdillahi Mutabazi - Mrajis Msaidizi Pwani
119. Ndg. John B. Henjewele - Mrajis Msaidizi Tanga
120. Ndg. Peja Mhoja - Mrajis Msiadizi Ruvuma
121. Ndg. Dotto S. Kanyoro - Meneja wa Kanda ZIC
122. Ndg. Pastory S. Ndalahwa - Afisa wa Bunge Wizara ya Kilimo
123. Dkt. Wilson Nene - Mtafiti TARI Naliendele
124. Ndg. William Mbasa - Mtafiti TARI Naliendele
125. Ndg. Bakari Kidunda - Mtafiti TARI Naliendele
126. Ndg. Stella M. Andrea - Mtafiti TARI Naliendele
127. Ndg. Mahmood Shoo - Mkurugenzi Bizytech Ltd
128. Ndg. Kondrad Shio - Mtafiti TASAC
129. Ndg. Emmanuel H. Hezron - kny CG TRA
130. Ndg. George K. Bokki - AD CO Wizara ya Kilimo
131. Ndg. Ferdinand Nyathi - Meneja Bandari Mtwara
132. Ndg. Irene Mwanga - Afisa TRA
133. Ndg. Faraji Mbulialina - Mkuu wa Idara Masoko Bandari
134. Ndg. Boniface Ngowi - Afisa ROTAI
135. Ndg. Joash Mutai - Afisa ROTAI
136. Ndg. Adelina Peter - Mkufunzi UDOM
137. Ndg. Abubakar Ndwata - RSM WRRB
138. Dkt. Aloyce Mbijilo - Mkurugenzi wa Tawi BOT- Mtwara
139. Ndg. Shadrack Mtunh - PRM CRDB Benki

**WASAMBAZAJI PEMBEJEO**

140. Ndg. Lucas Kauki - Meneja Kanda Meru Agro

**VYAMA VIKUU VYA USHIRIKA**

141. Ndg. Ismail M. Nalinga - Mwenyekiti Lindi Mwambao
142. Ndg. Karimu Chipola - Mwenyekiti TANECU
143. Ndg. Mohamedi Mwinguku - Meneja Mkuu TANECU
144. Ndg. Mlosa H. Mngeresa - Mwenyekiti CORECU

145. Ndg. Hassan E. Tawachi - Mwenyekiti MAMCU
146. Ndg. Nurdin S. Swallah - Meneja Mkuu Lindi Mwambao
147. Ndg. Biadia Matipa - Meneja Mkuu MAMCU
148. Ndg. Odasi O. Mpunga - Mwenyekiti RUNALI
149. Ndg. Jahida Hassan - Meneja Mkuu RUNALI
150. Ndg. Meshack Opulakwa - Katibu DOMASICA
151. Ndg. Marcelino Mrope - Meneja Mkuu TAMCU

**WAKULIMA**

152. Ndg. Masudi Rajabu Ummi - Mkulima Masasi
153. Ndg. Hasani Yusufu Mzungu - Mkulima Kilwa
154. Ndg. Ahmadi A. Yususfu - Mkulima Kilwa
155. Ndg. Maurus Petro - Mkulima Ruangwa
156. Ndg. Hamisi Mbalapi - Mkulima Newala
157. Ndg. Issa I. Ajabu - Mkulima Newala Mji
158. Ndg. Hanafi N. Nahonyo - Mkulima Newala
159. Ndg. Raufu H. Matumla - Mkulima Mkuranga
160. Ndg. Mbwana M. Mwaroho - Mkulima Mkinga
161. Ndg. Antonio R. Shayo - Mkulima Liwale
162. Ndg. Ally A. Mohamedy - Mkulima Ruangwa
163. Ndg. Issah Rashid Madenge - Mkulima Manyoni
164. Ndg. Bakari H. Milanzi - Mkulima Nanyumbu
165. Ndg. Mussa a. Ngarabuke - Mkulima Rufiji
166. Ndg. Ibrahim a. Mkweche - Mkulima Tandahimba
167. Ndg. Charles m. Gregory - Mkulima Masasi
168. Ndg. Rajabu Ngombwele - Mkulima Mtama
169. Ndg. David V. Kyungu - Mkulima Masasi
170. Ndg. Adinani M. Maluka - Mkulima Nachingwea
171. Ndg. Avithius P. Sendeu - Mkulima Nachingwea
172. Ndg. Izack Renald Chee - Mkulima Ruangwa
173. Ndg. Juma H. Mohamedi - Mkulima Tandahimba
174. Ndg. Nurudini Rashid - Mkulima Newala
175. Ndg. Hago Mohamedi - Mkulima Newala
176. Ndg. Ally R. Mkwaya - Mkulima Kibiti

| | | | |
|---|---|---|---|
| 177. | Ndg. Malimus Kasembe Abdallah | - | Mkulima Masasi |
| 178. | Ndg. Rashidi R. Namanjoya | - | Mkulima Tandahimba |
| 179. | Ndg. Mahamudu Lupanda | - | Mkulima Mtwara Manispaa |
| 180. | Ndg. Abdalah S. Sayuki | - | Mkulima Tandahimba |
| 181. | Ndg. Hassan Ally Mahauji | - | Mkulima Nanyamba |
| 182. | Ndg. Shaibu Jamadin | - | Mkulima Tunduru |
| 183. | Ndg. Rashidi Mbalamla | - | Mkulima Tunduru |
| 184. | Ndg. Hassan Y. Mpako | - | Mkulima Liwale |

**WANUNUZI, WAENDESHA GHALA NA WASAFIRISHAJI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 185. | Ndg. Inviolate Tango | - | Afisa Manunuzi Maersk |
| 186. | Ndg. Rogers Kessi | - | Afisa Maersk |
| 187. | Ndg. Salum Mkemi | - | Mwenyekiti Umoja wa Wanunuzi |
| 188. | Ndg. Omega Menas | - | Katibu wa Wanunuzi |
| 189. | Ndg. Fatina Masungwa | - | Mnunuzi |
| 190. | Ndg. Rehema Wilson | - | Mwenyekiti Waendesha Ghala |
| 191. | Ndg. Doreen Njau | - | Katibu Waendesha Ghala |
| 192. | Ndg. Paul Felix | - | Mwenyekiti Usafirishaji |

**WABANGUAJI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 192. | Ndg. Bahati Mayoma | - | Mwenyekiti TACP |
| 193. | Ndg. Daniel Marwa | - | Mhasibu TACP |
| 194. | Ndg. Aqlhassan Satya | - | Mapato TACP |

**MENEJIMENTI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 195. | Ndg. Francis Alfred | - | Mkurugenzi Mkuu |
| 196. | Ndg. Reuben Putaputa | - | Kaimu Mkurugenzi wa Fedha naUtawala |
| 197. | Ndg. Revelian Ngaiza | - | Kaimu Mkurugenzi Masoko na Udhibiti Ubora |
| 198. | Ndg. Juma Yusuph | - | Kaimu Meneja Mipango ya Kilimo |
| 199. | Ndg. Sumwike Kajela | - | Mkuu wa Kitengo cha Ugavi na Manunuzi |
| 200. | Ndg. Mangile Malegesi | - | Kaimu Meneja Ubanguaji |
| 201. | Ndg. Francis H. Kugesha | - | Katibu wa Sheria |
| 202. | Ndg. Ray Mtangi | - | Kaimu Meneja wa Tawi Manyoni |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 204. | Ndg. Salum Khalifa | - | Kaimu Meneja Masoko |
| 205. | Ndg. Joseph Nyumayo | - | Mhasibu |
| 206. | Ndg. Juma Matayi | - | Kaimu Mhasibu Mkuu |
| 207. | Ndg. Gerald Rogathe | - | Kaimu Mkuu wa Kitengo TEHAMA |
| 208. | Ndg. Jasper Kiwia | - | Afisa Ubora |
| 209. | Ndg. Zuberi A. Mshamu | - | Kaimu Meneja Utumishi na Utawala |
| 210. | Ndg. Birahi Kitang'ita | - | Mkaguzi wa ndani |
| 211. | Ndg. Shaban N. Hamis | - | Mkaguzi wa ndani |
| 212. | Ndg. Salama Wakati | - | Mwandishi Mwendesha Ofisi |
| 213. | Ndg. Grace Mahundu | - | Mwandishi Mwendesha Ofisi |

**WAANDISHI WA HABARI**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 214. | Ndg. Mohamed Mwaya | - | Kusini Yetu |
| 215. | Ndg. Mohamed Kemkem | - | Mtwara Online |
| 216. | Ndg. Valentine Ofuo | - | Guardian Ltd |
| 217. | Ndg. Peter Mkwavila | - | Nipashe |
| 218. | Ndg. Ramadhan Hassan | - | Mtanzania Digital |
| 219. | Ndg. Aden Kinyaha | - | Sema Tv |
| 220. | Ndg. Sharifa Mdeme | - | Clouds Tv |
| 221. | Ndg. Sijawa Omari | - | Habari Leo |

**AJENDA**

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Kupitia Muhtasari wa kikao cha tathmini ya uzalishaji, Ubanguaji na masoko ya korosho kilichofanyika tarehe 24 Aprili, 2023.
4. Kupitia utekelezaji wa yatokanayo na kikao cha tathmini ya uzalishaji, ubanguaji na masoko ya korosho kilichofanyika tarehe 24 Aprili, 2023.
5. Kupokea taarifa ya tathmini ya uzalishaji, ubanguaji na masoko ya korosho msimu wa 2023/2024 na mipango ya msimu wa 2024/2025:
    a. Uzalishaji,
    b. Masoko, na
    d. Ubanguaji.

6. Taarifa ya maendeleo ya utafiti katika zao la korosho kutoka TARI Naliendele.
7. Taarifa kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) - Mtwara.
8. Taarifa kutoka Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi ya Ghala (WRRB).
9. Taarifa kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC).
10. Mengineyo.
11. Kufunga kikao.

## 1.0 KUFUNGUA KIKAO

Kabla ya Mwenyekiti kufungua kikao aliwakaribisha viongozi mbalimbali kutoa salam kwa wadau

### 1.1 Salamu za Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania

Brig. Gen. (Mstaafu) Aloyce D. Mwanjile *ndc* alianza kwa kutoa salaam kwa kuelezea mafanikio mbalimbali yaliyopatikana katika msimu wa 2023/2024 ikwa ni pamoja na: Kuongezeka kwa thamani ya pembejeo zilizosambazwa kwa wakulima kutoka shilingi **bilioni 96** msimu wa 2022/2023 hadi kufikia **bilioni 189** msimu wa 2023/2024; Kuongezeka kwa uzalishaji kutoka **tani 189,000** msimu wa 2022/2023 hadi kufikia **tani 305,000** msimu wa 2023/2024; Asilimia kubwa ya Wakulima kulipwa fedha zao ndani ya siku 7 za kazi baada ya mnada kufanyika; Kuuzwa kwa korosho ghafi asilimia 99 ya zilizopelekwa sokoni pamoja na mahitaji ya soko la nje kuwa madogo; Kusafirishwa kwa korosho **asilimia 97.7** ya korosho zote zilizosafirishwa kwenda nchi za nje kupitia bandari ya Mtwara baada ya agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan; na Kuhamasisha ubanguaji wa korosho kupitia vikundi vidogo vidogo ambapo jumla ya mashine 100 za kubangua korosho zilitolewa kwa vikundi vidogo vya kubangua korosho kutoka mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma.

Aidha, alielezea mipango ya msimu wa 2024/2025 ya kuongeza uzalishaji, ubanguaji na ufanisi wa masoko ya korosho hapa nchini kama ifuatavyo: Kuratibu na kusimamia upatikanaji wa pembejeo, mabomba na magunia kupitia Mradi wa Pamoja wa Vyama Vikuu vya Ushirika; Kutoa mafunzo ya kilimo bora cha korosho na matumizi sahihi na salama ya viuatilifu; Kuhuisha kanzidata ya wakulima wa korosho nchini kwa kupima mashamba; Kutoa mafunzo ya mbinu sahihi za uvunaji, uhifadhi, udarajishaji, uhakiki

ubora wa korosho ghafi na matumizi sahihi ya vipima unyevu kwa wakulima, maafisa ugani, viongozi wa AMCOS na wataalam wa ghala za minada; na Kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa kongani la viwanda vya kubangua korosho katika kijiji cha Maranje Mkoa wa Mtwara.

**1.2 Salamu za Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo**

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo, na Mifugo Mhe. Deodatus Mwanyika (MB) alitoa pongezi kwa Wizara ya Kilimo kwa juhudi kubwa ya kuendeleza zao la korosho nchini, kwa kulitambua zao la korosho kuwa la kimkakati kwani linaliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni. Alilisisitiza kuongeza juhudi za kuwadumia wakulima ili kufikia malengo ya uzalishaji, ubanguaji na masoko. Mwisho alishukuru kwa kupata fursa ya kuungana na wadau wengine katika kupanga mipango ya uendelezaji zao.

**1.3 Salamu za Mkuu wa Mkoa wa Dodoma**

Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa alitoa shukrani kwa Wizara ya Kilimo kwa kuendelea kuruhusu kufanyika vikao vya tathmini mkoani kwake. Alieleza kuwa Mkoa wa Dodoma unaendelea na mipango ya kulima zao la korosho. Aliwakaribisha wadau Mkoani Dodoma na kueleza kuwa Dodoma ni salama. Alimalizia kwa kueleza kuwa katika msimu wa mwaka 2023/2024 Mkoa utaendelea kutekeleza mipango ya kuendeleza Tasnia ya Korosho.

**1.4 KUFUNGUA KIKAO**

Kikao kilifunguliwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Ndg. Gerald Mweli *ndc* kwa niaba ya Mhe. Hussein M. Bashe (MB) Waziri wa Kilimo huku akieleza kuwa Mheshimiwa Waziri atachelewa kufika kwenye kikao kutokana na majukumu ya Bunge. Alieleza kuwa Wizara imeliweka zao la korosho kuwa moja ya mazao ya kimkakati na hivyo kama kila mdau akitimiza wajibu wake serikali itaweza kutimiza nalengo yake ikiwemo kuzalisha tani 1,000,000 ifikapo 2029/2030 na kufikia agenda 10/30. Alieleza kuwa Serikali imetoa fedha nyingi kwenye tasnia ya korosho kwa ajili ya kununua pembejeo hivyo hakuna sababu ya kutofikiwa malengo ya uzalishaji. Alihimiza Maafisa Kilimo kutoa elmu na ushauri sahihi na bora kwa wakulima ili waweze kuzalisha kwa tija na hivyo kujipatia kipato na kuongeza mapato ya Serikali.

Aliwapongeza na kuwashukuru wadau wa korosho wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakulima na wadau wengine kwa kufanikisha uzalishaji wa tani 305,000.

Alihimiza kuendelea kusimamia zao ikiwemo minada ya mauzo ya korosho kwani bila kuwepo kwa usimamizi imara bei ya zao itashuka kila wakati. Mwisho aliagiza watendaji kuwa na uadilifu ili kumwezesha mkulima kunufaika na zao lake. Allifungua kikao saa 4:42 asubuhi.

## 3.0 KUTHIBITISHA AJENDA

Wajumbe walithibitisha ajenda kama zilivyowasilishwa.

## 4.0 KUPITIA MUHTASARI WA KIKAO CHA TATHMINI YA UZALISHAJI NA MASOKO KILICHOFANYIKA TAREHE 24 Aprili, 2023

Wajumbe walipitia muhtasari wa kikao kilichofanyika tarehe 24 Aprili, 2023, kufanya masahihisho kwenye baadhi ya maneno na kuridhia kuwa ni kumbukumbu sahihi za kikao hicho.

## 5.0 KUPITIA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATHMINI YA UZALISHAJI NA MASOKO KILICHOFANYIKA TAREHE 24 APRILI, 2023

Wajumbe walipokea na kukubaliana na utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa kwenye kikao kilichofanyika tarehe 24 Aprili, 2023.

## 6.0 KUPOKEA TAARIFA YA TATHMINI YA UZALISHAJI, UBANGUAJI NA MASOKO YA KOROSHO MSIMU WA 2023/2024 NA MAANDALIZI YA MSIMU WA 2024/2025

### 6.1 UZALISHAJI WA KOROSHO GHAFI

Ilielezwa kuwa katika kipindi cha msimu wa 2023/2024 Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na wadau iliratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango mbalimbali iliyolenga kuongeza uzalishaji wa korosho ghafi nchini kutoka tani **189,113.799** zilizozalishwa msimu wa 2022/2023 hadi tani **400,000** msimu wa 2023/2024. Mipango hiyo ilikuwa ni pamoja na: Uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho; Usambazaji wa pembejeo za ruzuku za korosho; Mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu; na Usambazaji wa mbegu bora za korosho.

Ilifahamishwa kuwa Bodi ya Korosho iliratibu na kusimamia zoezi la uhuishaji wa kanzidata ya wakulima ambao ulihusisha upimaji wa mashamba ya mikorosho ya wakulima, kupiga picha za mkulima *(Passport size)*, na taarifa nyingine zinazohusiana na mkulima. Jumla ya wakulima 563,932 wenye jumla ya ekari 3,569,523.449 na

mikorosho 80,870,287 kutoka Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani na Tanga walihuisha taarifa zao. Aidha, jumla ya washiriki 69,725 wakiwemo maafisa ugani 452, wakulima na wapuliziaji 69,173 walipewa mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu vya zao la korosho.

**i. Usambazaji wa pembejeo za ruzuku za korosho**

Kuhusu kuratibu na kusimamia upatikanaji, usambazaji na ugawaji wa viuatilifu, mabomba na magunia katika zao la korosho kupitia Mradi wa Pamoja wa Vyama Vikuu vya Ushirika *(Korosho Cooperative Joint Enterprise Ltd – KCJEL)* ilielezwa kuwa lengo lilikuwa ni kusambaza *sulphur* ya unga tani 70,000 na viuatilifu vya maji lita 3,130,000 ili kumpunguzia mkulima gharama ya viuatilifu msimu wa 2023/2024 na pia kupata kianzio cha msimu wa 2024/2025. Kwa upande wa mabomba ilielezwa kuwa lengo lilikuwa kusambaza mabomba 5,250 na kwamba mkulima atalipia 50% ya bei ya bomba. Pia gunia lengo lilikuwa kusambaza magunia 4,600,000 pamoja na bakaa ya gunia 3,198,702 yaliyokuwepo kwenye Vyama vya Ushirika hivyo jumla kuwa na gunia 7,798,702.

Ilifahamishwa kuwa kuelekea msimu wa 2023/2024 Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele ilisambaza mbegu bora kilo 23,490 sawa na wastani wa miche 3,288,600 katika Mikoa 10 yenye jumla ya Halmashauri 36 zilizoomba mbegu kwa sharti la kuotesha miche na kuigawa kwa wakulima. Kufuatia mipango na jitihada mbalimbali zilizofanyika msimu wa 2023/2024 katika kuongeza uzalishaji wa korosho nchini hadi kufikia tarehe 18 Aprili, 2024 jumla ya tani 305,014.597 sawa na 76.25% ya lengo la kuzalisha korosho ghafi tani 400,000 zilikuwa zimepatikana.

Kuhusu mipango ya kuelekea msimu wa 2024/2025 kwa ajili ya maandalizi ya uzalishaji wa korosho ghafi ilikuwa ni uhuishaji wa kanzidata ya wakulima wa korosho nchini; Usambazaji wa pembejeo za ruzuku za korosho kwa wakulima; Mafunzo ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa wakulima; na Usambazaji wa mbegu bora za korosho kwa Halmashauri zilizokuwa tayari kuzalisha miche na kugawa kwa wakulima

## 5.2 UBANGUAJI WA KOROSHO NA USINDIKAJI WA BIDHAA ZAKE

Ilielezwa kuwa katika msimu wa mwaka 2023/2024 shughuli zilizotekelezwa ili kuongeza ubanguaji ilikuwa ni Pamoja na: Kuhamasisha ujenzi wa viwanda ili kuongeza ubanguaji wa korosho ndani ya nchi ambapo kiwanda kipya cha kampuni ya TC

Agriculture Company Ltd chenye uwezo wa kubangua tani 4,800 za korosho ghafi kimefunguliwa; Mafunzo ya ubanguaji wa korosho yametolewa kwa watu wenye ulemavu 45 na vijana 65 wa Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mtwara; Kuanza kwa mradi wa kongani la viwanda kijiji cha Maranje Mkoa wa Mtwara ambapo kazi zilizokuwa zimefanyika ni kutwaa eneo la ekari 354, kulipa fidia, kusafisha na kupanga viwanja vya uwekezaji kwenye eneo. Utekelezaji wa shughuli hizo kwa mwaka mzima ulifanikisha ubanguaji wa korosho kuongezeka kufikia tani 26,656 kutoka tani 11,970 za msimu wa 2022/2023.

Ilifahamishwa kuwa mipango ya kuongeza ubanguaji wa korosho nchini ilikuwa: Kuendeleza ujenzi wa kongani la viwanda katika kijiji cha Maranje Mkoa wa Mtwara; Kutoa mafunzo ya kanuni bora za ubanguaji wa korosho; na Kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda vya kubangua korosho

**5.3 MASOKO YA KOROSHO**

Ilielezwa kuwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2024 jumla ya minada 55 ilikuwa imefanyika na korosho ghafi kiasi cha tani 244,646.026 zilikuwa zimeuzwa katika ghala za minada zikiwa na thamani ya shilingi 454,016,863,103. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2024, bei ya mauzo ya korosho ghafi katika minada ilikuwa kati ya shilingi 1,840/= hadi 2,200/= kwa kilo kwa korosho zenye ubora wa daraja la kwanza na shilingi 900/= hadi 1,500/= kwa kilo kwa korosho zenye ubora wa daraja la pili. Hivyo wastani wa bei kwa daraja la kwanza ilikuwa ni shilingi 1,874/= na shilingi 1,213/= kwa daraja la pili.

Ilifahamishwa kuwa hali ya ubora wa korosho ghafi zilizoingia kwenye mfumo wa mauzo kwa msimu 2023/2024 ilishuka kwa asilimia 0.5 kutoka 99% ya korosho daraja la kwanza msimu 2022/2023 hadi asilimia 98.5 ya korosho daraja la kwanza.

Kuhusu mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na wakulima kulipwa fedha zao ndani ya siku 7 za kazi baada ya mnada kufanyika. Korosho ghafi tani **236,149.95** sawa na asilimia **94.7** ya korosho zote zilizosafirishwa kwenda nchi za nje zilipitia Bandari ya Mtwara baada ya agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Kuhusu mipango ya masoko msimu wa 2024/2025 ilikuwa: Kutoa mafunzo ya udhibiti ubora kuanzia ngazi ya mkulima na ngazi ya AMCOS; Kutoa mafunzo kwa wadhibiti

ubora katika ngazi ya ghala kuu na ghala za AMCOS; Kuingia mkataba na Halmashauri kuwatumia waratibu wa zao la korosho katika kusimamia ubora ngazi ya ghala kuu za mnada; Kuwa na kanzidata ya wabanguaji wadogo katika ngazi ya Halmashauri ili kudhibiti mauzo ya korosho karanga; Kushawishi wawekezaji kujenga ghala katika Manispaa ya Mtwara ili kuondoa changamoto za uhifadhi wa korosho wakati wa masafirisho nje ya nchi kupitia Bandari; Kutoa mafunzo kwa wabanguaji wadogo, wa kati na wajasiriamali wadogo juu ya uhifadhi wa korosho karanga ili kutunza ubora na Kuhamasisha ulaji wa korosho nchini.

## 6.0 TAARIFA YA MAENDELEO YA UTAFITI KATIKA ZAO LA KOROSHO

Ilitaarifiwa kuwa kilimo cha Korosho kama ilivyo kwenye mazao mengine hukabiliana na changamoto mbalimbali ambazo huhitaji kufanyiwa utafiti na kupatiwa suluhisho. Jukumu la utafiti kitaifa kwenye zao la korosho hutekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kituo cha Naliendele. TARI kituo cha Naliendele imekuwa ikishirikiana na watafiti walioko vituo vingine vidogo kama ifuatavyo: Kiituo kidogo (Sub-station) cha Mkumba kilichopo katika wilaya ya Nachingwea; Kituo cha majaribio (trial site) cha Mtopwa kilichopo wilayani Newala; na Vituo vya uendelezaji zao la korosho (cashewnut development centres, CDCs), ambavyo ni:- Nyangao (Lindi Vijijini), Nanyanga (Tandahimba), Nakayaya (Tunduru), Mkuranga (Mkuranga), Mkumba (Nachingwea), Mtopwa (Newala) na Chambezi (Bagamoyo).

Ilifahamishwa kuwa mafanikio ya utafiti wa zao la korosho ni pamoja na: Kuzalisha miche 239,762 na kilo 30,380 sawa na tani 30.38 za mbegu bora; Ilielezwa kuwa, mbegu aina nane (8) bora za Korosho ambazo ni kinzani dhidi ya ugonjwa wa blaiti zinatarajiwa kupendekezwa kwa wakulima mwaka 2024 kwa ajili ya matumizi. Ilielezwa kuwa aina hizo za mbegu kwa sasa zilikuwa katika hatua ya mwisho na TOSCI walikuwa wanazifanyia kazi kwa ajili ya kuzithibitisha; Kuanzisha mashamba ya mfano 30 kwa ajili ya kufundishia teknolojia mbalimbali za zao la korosho; Kuendelea kusimamia mashamba ya mbegu *(Polyclonal Seed Garden)* yakiwemo mashamba mapya katika wilaya ya Mkinga (ekari 20) na Pangani (ekari 30) mkoani Tanga; Kuendelea kufanya ufuatiliaji kwa mashamba darasa kumi na nne (14) yaliyoanzishwa katika maeneo ya Mpwapwa, Mkoka, Makutupora, Itigi, SUA, Mbalali, Chemba, Singida, Manyoni, Gairo, Mlele Katavi na Mkuranga; Kuendelea kutunza benki kubwa ya vinasaba vya korosho kutoka kwenye mashamba ya TARI na majaribio zikiwemo aina 54 zilizosajiliwa, 6 za nje ya nchi na 4 za ndani ya nchi; na Kutoa mafunzo ya kilimo

bora cha zao la korosho kwa washiriki wapatao 2,556 ambapo ndani yake kulikuwa na maafisa ugani (806), wakulima (1,482) pamoja na wadau wengine wapatao 268 walipata elimu kupitia njia mbalimbali.

Aidha, zilielezwa changamoto mbalimbali zinazokabili uzalishaji wa zao la korosho ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya tabia nchi na mapendekezo ya utatuzi wake.

## 7.0 TAARIFA YA USAFIRISHAJI WA KOROSHO GHAFI KUTOKA MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BANDARI TANZANIA (TPA) – MTWARA

Ilielezwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya ziara Mkoani Mtwara ambapo tarehe 15 Septemba, 2023 alitembelea Bandari ya Mtwara na kuelekeza kuwa katika msimu wa mwaka 2023/2024, korosho zote zinazozalishwa katika Mikoa ya Kusini zisafirishwe kupitia Bandari ya Mtwara.

Baada ya agizo hilo, Bandari ya Mtwara ikajipanga ambapo hadi tarehe 21 Februari 2024 jumla ya meli **28** zilihudumiwa na Makasha Matupu **8,700** yalipokelewa kutoka kampuni mbalimbali za meli huku makasha **1,182** yakiwa ya ukubwa wa futi 20 na makasha **7,518** yakiwa ya ukubwa wa futi 40. Aidha, jumla ya makasha **4,572** ya ukubwa wa futi 40 na makasha **725** ya futi 20 yalisarifishwa kwenda nchini India na jumla ya makasha **2,512** ya ukubwa wa futi 40 na makasha **158** ya futi 20 yalisarifishwa kwenda nchini Vietnam.

Hivyo hadi kumalizika kwa msimu wa korosho kwa mwaka 2023/2024, Bandari ya Mtwara ilifanikiwa kuhudumia jumla ya makasha **29,522 (TEUS)** na kusafirisha Jumla ya **tani za mapato 253,616.94.** Aidha, jumla ya makasha **2,716 (TEUS)** ya makampuni ya Meli ya CMA – CGM na MSC yaliondoka Bandarini yakiwa matupu bila ya shehena ya korosho.

## 8.0 TAARIFA KUTOKA BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI YA GHALA

Ilielezwa kuwa katika msimu wa mwaka 2023/2024 Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala ilitoa jumla ya leseni arobaini na sita (46); katika mikoa mitano (5) ya Lindi, Mtwara, Pwani, Ruvuma na Morogoro kwenye jumla ya wilaya kumi na nane (18) zinazozalisha korosho*.* Kuhusu makusanyo ilielezwa kuwa **k**atika msimu wa 2023/2024 jumla ya kilogramu 244,573,341 zilikusanywa ambapo mkoa wa Lindi (68,786,662), Mtwara (139,160,700), Pwani (10,546,232), Ruvuma (26,079,747) na Morogoro

(196,800). Aidha kati ya kilogramu 244,573,341 zilizopokelewa ulilipotiwa upungufu wa kilogramu 1,775,262 sawa na asilimia 0.73% ya mzigo wote ambapo ulisababisha kuwepo kwa madai ya thamani ya Tshs. 2,878,101,343.00. Kiwango hiki kilikuwa sawa na 33% ya hatari iliyokokotolewa ambayo inaweza kutokea kwa kuzingatia mkataba wa Sera ya Kinga ya Utendaji iliyokuwa na thamani ya kuweza kulipa Tsh. 8,770,000,000.

Ilifahamishwa kuwa hadi kuelekea mwisho wa msimu, NIC ilifanikiwa kulipa kiasi cha Tsh. 348,605,159.00 ya madeni yote ambayo ni sawa na asilimia 12% pekee ya madai yaliyojitokeza na kiasi kilichobaki madai yanaendelea kufuatiliwa ili kukamilisha ulipaji wake; ambapo kwa wakati huo sharti hilo lilikuwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA).

## 9.0 TAARIFA KUTOKA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA

Ilielezwa kuwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ina jukumu la kuhamasisha na kusimamia shughuli za Vyama vya Ushirika nchini na katika Vyama vya Korosho. Tume ilitekeleza majukumu yafuatayo: Kutoa waraka wa Usimamizi wa Biashara na masoko ya Korosho kila msimu; Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kuandaa Mwongozo wa Mauzo ya Korosho kila Mwaka; Kuratibu na kuhakikisha kuwa Vyama vya ushirika vinakuwa na vifaa na vitendea kazi kama vile vitabu vya Stakabadhi za ghala, Mizani na Vifungashio kipindi cha msimu; Kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa mara kwa mara hususani kipindi cha msimu wa mauzo ya korosho; Kuhakikisha Vyama vya Ushirika vinawalipa wakulima kwa wakati baada ya mauzo; Kuhakikisha Vyama vya Ushirika vinahakiki mizani za kupimia korosho kabla ya kuanza kwa msimu; Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kuratibu mafunzo ya Ubora wa korosho kwa makarani wapimaji; Kuhamasisha na kuratibu upatikanaji na matumizi ya mizani za kidigitali pamoja na Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika kielektroniki (MUVU); na Kutatua migogoro mbalimbali ambayo ilijitokeza kipindi cha mauzo.

Aidha, katika msimu 2023/2024 Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilisimamia Vyama vya Ushirika vipatavyo 759 katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Pwani, Tanga, Morogoro, Singida, Dodoma, Songwe na Mbeya. Katika utekelezaji huo, Tume ilifanya kazi zifuatazo: Kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho, Tume iliandaa mwongozo wa Mauzo ya Korosho msimu 2023/2024; Kutoa Waraka wa Usimamizi kwa Vyama vya Ushirika vya Korosho Nchini; Kusimamia kikamilifu malipo ya Fedha za mauzo ya Korosho kwenda kwa wakulima; Kusimamia mauzo ya korosho kupitia minada iliyokuwa

inafanyika kwa uratibu wa Vyama vikuu; Kushirikiana na wadau wengine kusimamia mauzo ya korosho kupitia soko la awali; Kusimamia kikamilifu ununuzi wa vifungashio/gunia kupitia Vyama vya Ushirika; na Kuratibu na kusimamia upatikanaji na ugawaji wa pembejeo. Aidha, zilitolewa changamoto mbalimbali zilizojitokeza na mapendekezo ya utatuzi wake ikiwa ni pamoja na mikakati ya utekelezaji kwa msimu wa 2024/2025.

**10.0 MENGINEYO**

Hakukuwa na mengineyo

**11.0 KUFUNGA KIKAO**

Mgeni Rasmi aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki kikamilifu na kutoa michango ya mawazo itakayosaidia katika kuendeleza Tasnia ya Korosho nchini. Aidha, aliwashauri wadau wa zao la korosho kujielekeza katika kufanya kazi ili kufanikisha uzalishaji wa korosho kufikia tani 700,000 ifikapo 2025/2026 na tani 1,000,000 ifikapo 2029/2030 ili kuongeza mchango wa zao la korosho katika kufikia ajenda 10/30. Kikao kilifungwa saa 12:35 jioni.

Muhtasari huu umethibitishwa leo tarehe…………………………………..………..

**………………………..** **…………………………..…**

**MWENYEKITI** **KATIBU**

**AGENDA NA. 4: KUPITIA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATHMINI YA UZALISHAJI, UBANGUAJI NA MASOKO YA KOROSHO KILICHOFANYIKA TAREHE 22 APRILI, 2024**

**KUPITIA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATHMINI YA UZALISHAJI, UBANGUAJI NA MASOKO YA KOROSHO KILICHOFANYIKA TAREHE 22 APRILI, 2023**

| NA | HOJA | MAAZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Upatikanaji wa pembejeo za msimu wa 2023/2024 | Pembejeo zigawiwe zikiwa na QR code za kieletroniki | TPHPA na CBT | Katika msimu wa 2024/2025 pembejeo ziligawiwa kwa wakulima kupitia mfumo wa kiditali zikiwa na QR code za kietroniki. |
| | | Pembejeo zitolewe kwa wakulima kwa ruzuku ya asilimia 100. Aidha, pembejeo hizo ni ruzuku ya Serikali Wakulima watapaswa kujinunulia pembejeo iwapo zinazotolewa bure na Serikali hazitatosheleza. | CBT | Pembejeo za msimu wa 2024/2025 zilitolewa bure (ruzuku 100%) bila wakulima kuchangia gharama. |
| 2 | Kuongeza tija na uzalishaji | Bodi ya Korosho Tanzania iajiri Maafisa Ugani ili waweze kuhudumia wakulima | Wizara ya Kilimo na CBT | Bodi ya Korosho Imeajiri vijana 500 kupitia mpango wa BBT Korosho na kuwagawa kwenye kata zinazolima korosho kwenye Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma (Tunduru), Pwani na Tanga. Aidha, vijana hawa wamepewa pikipiki na vishikwambi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha. |
| 3 | Masoko ya Korosho | Korosho, ufuta na mbaazi viuzwe kupitia mfumo wa Soko la Bidhaa | CBT, TMX, WRRB, TCDC | Katika msimu wa 2024/2025 zao la korosho limeuzwa kupitia mfumo wa Soko la Bidhaa Tanzania |

| NA | HOJA | MAAZIMIO | MHUSIKA | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|---|
| | | Leseni za kununua korosho zitolewe kwa kampuni na mkurugenzi mmoja | CBT | Katika msimu wa 2024/2025 leseni za kununua korosho zimetolewa kwa kampuni na Mkurugenzi mmoja na siyo Mkurugenzi mmoja kumiliki kampuni zaidi ya moja. |
| | | Wabanguaji wa ndani wanunue korosho kupitia Bodi ya Korosho kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika | CBT na TCDC | Katika msimu wa 2024/2025 wabanguaji wa ndani walinunua korosho baada ya kutambulishwa na Bodi ya Korosho Ofisi za Katibu Tawala wa Mikoa, Ofisi za Wakurugenzi wa Halmashauri na kupangiwa. |
| | | Zabuni ya usafirishaji wa korosho ghafi itangazwe ili kupata mzabuni mwenye gharama nafuu | TCDC, UNION | Zabuni za usafirishaji wa korosho ghafi kutoka kwenye ghala za AMCOS kwenda kwenye ghala za minada zilitangazwa ambapo wazabuni wenye gharama ndogo walipewa kazi ya kusafirisha korosho. |
| 4 | Taarifa ya kamati ya Uchunguzi | Mtumishi wa Bodi ya Korosho anayetuhumiwa kukihuka taratibu za kuitumishi asimamishwe kazi ili kupisha uchunguzi | CBT | Mtumishi alisimamishwa kazi na taratibu za kuichunguzi zilifanyika na maamuzi kutolewa kwa kuzingatia kanuni za Utumishi wa Umma. |
| | | Wakati wa uhuishaji wa kanzidata ya wakulima redio za kijamii zitumike ili wakulima waweze kupata taarifa juu ya kufanyika kwa zoezi hli | CBT na LGA | Katika msimu wa 2024/2025 zoezi la uhuishaji wa kanzidata ya wakulima lilihusisha matumizi ya redio za kijamii ili kuwapa wakulima taarifa juu ya utekelezaji wa zoezi hilo. |

**AGENDA NA. 5: KUPOKEA TAARIFA YA TATHMINI YA UZALISHAJI, UBANGUAJI NA MASOKO YA KOROSHO MSIMU WA 2024/2025 NA MIPANGO YA MSIMU WA 2025/2026**

## 5.0 UTEKELEZAJI WA MIPANGO MSIMU WA MWAKA 2024/2025 NA MIPANGO YA MSIMU WA MWAKA 2025/2026

### 5.1 UTEKELAZAJI WA MIPANGO MSIMU WA MWAKA 2024/2025

Katika msimu wa mwaka 2024/2025 malengo yalikuwa kuzalisha korosho ghafi tani 595,000, ubanguaji asilimia 50 na kuendelea kutafuta masoko ya uhakika na endelevu ya korosho na bidhaa zake ndani na nje nchi ili mkulima na wadau wengine waendelee kupata faida kutoka kwenye zao la korosho. Hivyo, katika kufikia malengo hayo Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa Tasnia imetekeleza mipango na mikakati mbalimbali ikiwemo:

#### 5.1.1 KILIMO

##### 5.1.1.1 Kuratibu usambazaji wa pembejeo za ruzuku

Jumla ya tani 41,263 za *sulphur* na viuatilifu vya maji lita 2,689,581 vilisambazwa kwa wakulima kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao la korosho. Kiasi cha pembejeo kilichosambazwa ni sawa na asilimia 138 ya lengo la kusambaza sulphur tani 30,000 na asilimia 70 ya lengo la kusambaza viuatilifu vya maji lita 3,800,000. Pia, Bodi ya Korosho iliratibu usambazaji wa bakaa ya mabomba 543 ya kupulizia mikorosho yaliyobaki msimu wa 2023/2024. Mabomba hayo yalisambazwa kwa ruzuku ya asilimia 50 ambayo ni sawa na shilingi 390,000.00 kwa bomba chapa *shogun* na shilingi 597,500.00 kwa bomba chapa *pulmic take control*.

##### 5.1.1.2 Kuratibu usambazaji wa mbegu/miche bora ya mikorosho

Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania Kituo cha Naliendele (TARI Naliendele) imeratibu na kusambaza mbegu bora za korosho kilogramu 11,710 sawa na miche 1,639,400 na miche bora ya mikorosho 720,931 kwa Halmashauri zilizowasilisha mahitaji kwa ajili ya kuigawa kwa wakulima wao. Lengo katika msimu wa 2024/2025 lilikuwa kusambaza jumla ya miche 1,000,000 ya mikorosho. Hivyo, utekelezaji ni sawa na asilimia 236 ya lengo.

##### 5.1.1.3 Kuhuisha kanzidata ya wakulima wa zao la korosho nchini

Uhuishaji wa Kanzidata za wakulima unaratibiwa na Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazolima zao la korosho nchini. Aidha, zoezi hili kwa msimu wa 2024/2025 limetekelezwa na Maafisa Kilimo wa BBT Korosho kwa kushirkiana na Maafisa Ugani Kilimo ngazi ya Kata/Tarafa wa Halmashauri na Vyama Vikuu vya Ushirika ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2025 jumla ya wakulima 462,228 sawa na asilimia 77 ya lengo tarajiwa la wakulima 598,246 wamehuisha taarifa zao. Hata hivyo, bado zoezi la uhuishaji wa taarifa za wakulima linaendelea na linakwenda sambamba na ugawaji wa pembejeo kwa ajili ya uzalishaji wa korosho msimu wa 2025/2026.



*Maafisa kilimo wa BBT-KOROSHO wakiendelea na zoezi la uhuishaji taarifa za wakulima wa korosho wilayani Mtama mkoani Lindi.*

#### 5.1.1.4 Kuratibu upatikanaji wa huduma za ugani kwa wakulima

Maafisa Ugani 419 walipata mafunzo rejea ya matumizi sahihi na salama ya viuatilifu yaliyoratibiwa na Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele. Vile vile, wakulima 30,950 walipata mafunzo ya namna bora ya kutumia viuatilifu vinavyosambazwa na Serikali kwenye vituo vya kugawia pembejeo ili kuimarisha matumizi na ufanisi katika kudhibiti visumbufu vya zao la korosho sanjari na kupunguza athari katika mazingira. Vile vile, mafunzo yaliweza kutolewa kwa njia ya mitandao ya kijamii na kupitia vipindi vya redio jamii zikiwemo Ruangwa FM; Fadhila FM na Mamu FM za Masasi; Newala FM Newala; Hopaje FM na Safari FM za Mtwara; Mashujaa FM ya Lindi; Mercy FM ya Tunduru; Rufiji FM ya Pwani; na Maarifa FM ya Tanga.

### 5.1.2 UBANGUAJI

#### 5.1.2.1 Kuhamasisha ujenzi wa viwanda ili kuongeza ubanguaji wa korosho ndani ya nchi

Katika mwaka wa 2024/2025 ujenzi wa viwanda vipya umefanyika ikiwa ni pamoja na kiwanda kipya cha kampuni ya TANECU Ltd chenye uwezo wa kubangua tani 3,000 za korosho ghafi na kiwanda cha TC Agriculture Company Ltd chenye uwezo wa kubangua tani 5,000 vyote vikiwa vinabangua.

#### 5.1.2.2 Kutoa mafunzo ya ubanguaji bora wa korosho na usindikaji wa bidhaa zake

Mafunzo ya ubanguaji wa korosho yametolewa kwa vikundi vya Mikoa ya Mtwara, Lindi na Tanga ambapo jumla ya washiriki walikuwa 150. Pia jumla ya mashine 66 za

ubanguaji zimegawiwa vya vikundi vya ubanguaji wa korosho. Aidha, mafunzo ya umahiri kwenye zao la korosho awamu ya 20 (Master Training Programme – MTP 20) yametolewa kwa washiriki 64 wa mnyonoro wa thamani kutoka nchi 9 za Bara ya Afrika ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Ruanda, Burundi, Msumbiji, Zambia, Malawi na Sudani ya Kusini. Mafunzo haya yalifanyika katika Hotel ya Four Points By Sheraton kuanzia tarehe 24 – 28 Machi 2025.




*Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Korosho Tanzania* ***ndg. Francis Alfred*** *akikabidhi mashine nne za kubangulia korosho kwa Mstahiki Meya wa Manispaa ya Mtwara* ***Mhe. Shadida Ndile*** *na diwani wa viti maalum* ***Mhe. Zuhura Mikidadi.***

**5.1.2.3 Kukagua viwanda vya kubangua korosho**

Ukaguzi wa viwanda vya kubangua korosho umefanyika kwenye jumla ya viwanda 43 na kupewa leseni za kubangua korosho. Ukaguzi unafanyika ili kuhakikisha kuwa viwanda vinafanya kazi kwa kuzingatia sheria za nchi na kuzalisha bidhaa zenye ubora kitaifa na kimataifa.

### 5.1.2.4 Kuendelea na Ujenzi wa Mradi wa Kongani la Viwanda Kijiji cha Maranje Mkoa wa Mtwara

Bodi ya Korosho Tanzania imeendelea kutekeleza mradi wa kongani la viwanda vya kubangua korosho na kuongeza thamani mazao mengine yanayopatikana Mikoa ya Kusini. Kongani ili limeandaliwa kwa ajili ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Lengo ni kuwa na viwanda vya pamoja vitakavyofanikisha kubangua asilimia 100 ya korosho ya Tanzania ifikapo 2030 ili kufikia agenda 10/30. Kongani hili litakuwa na viwanda vya kubangua korosho, kusindika mafuta ya ganda la korosho na kuzalisha bidhaa mbalimbali zitokanazo na korosho. Aidha, kutakuwa na sehemu ya mafunzo kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wakubwa. Kongani linatarajiwa kutoa ajira zaidi ya 35,000 za moja kwa moja.

Kazi zilizofanyika katika eneo la ekari 354 ni kuandaa maeneo ya uwekezaji yenye ukubwa wa ekari 25 kila moja, kujenga ghala mbili zenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 kila mmoja ambapo ujenzi umefkia asilimia 50, kutafiti na kuchimba kisima cha maji, kusambaza umeme, kujenga barabara kwa kiwango cha changarawe zenye urefu wa kilomita 7.5 ambapo ujenzi uko ailimia 10.



*Naibu Katibu Mkuu Dkt Omary Hussein akikagua Ujenzi wa Mradi wa Kongani la Viwanda Kijiji cha Maranje Halmashauri ya Mji Nanyamba Mkoani Mtwara ukiendelea.*

### 5.1.3 UBORA

### 5.1.4 UDHIBITI UBORA

#### 5.1.4.1 Kutoa Mafunzo ya Udhibiti Ubora wa Korosho Ghafi kwa wakulima, viongozi wa AMCOS na wataalam ghala za mnada kabla ya kuanza msimu.

Bodi ya Korosho Tanzania imeatoa mafunzo ya mbinu sahihi za uvunaji, uhifadhi na uhakiki ubora kwa wataalam 150 wakiwemo mameneja wa ghala za mnada, viongozi wa AMCOS 1,526 katika Mkoa wa Mtwara, Lindi, Pwani, Tanga na Morogoro na wakulima 2,979 katika Wilaya zilizokuwa na changamoto za ubora msimu uliopita. Aidha elimu ya udhibiti ubora pia ilitolewa kwenye redio na mitandao ya kijamii.




*Mafunzo ya ubora kwa vitendo yakitolewa kwa washiriki*

#### 5.1.4.2 Kufanya Ukaguzi ghala za AMCOS na Ghala za Minada

Msimu 2024/2025 ukaguzi umefanyika kwa ghala za mnada 45 zilitumika kuhifadhi korosho ghafi na ghala za AMCOS zaidi ya 90 zilizokuwa na changamoto za ubora wa korosho ghafi wakati wa msimu lengo  ikiwa kuhakikisha kuwa taratibu, miongozo, kanuni na sheria kuhusiana na ubora wa korosho ghafi inazingatiwa ipasavyo.

#### 5.1.4.3 Kusimamia Mapokezi na Utoaji wa Korosho Ghafi kwenye Ghala za Mnada

Msimu 2024/2025 Bodi ya korosho Tanzania iliweka wataalam katika ghala la mnada kwa lengo la kuhakikisha wanasimamia mapokezi ya korosho ghafi, zoezi la uhakiki ubora na utoaji wa korosho zenye ubora  wakati wote wa msimu kwa mujibu wa Sheria ya Tasnia ya korosho na Mwongozo na 2 wa Usimamizi na Udhibiti Ubora wa korosho ghafi msimu 2024/2025. Aidha wataalam hawa walitatua migogoro ya ubora kati ya wanunuzi na waendesha ghala, Vyama vya Msingi na waendesha ghala wakati wote wa msimu.



*Kaimu Mkurugenzi wa Masoko na Udhibiti Ubora,* ***Revelian Ngaiza****,(wa tatu kushoto) akikagua shughuli za ushafirishaji wa zao la korosho katika ghala la Export lililopo wilayani Nachingwea mkoani Lindi, katika msimu wa 2024/2025.*

### 5.1.5 MASOKO

#### 5.1.5.1 Kuratibu ukusanyaji na uuzaji wa korosho ghafi kupitia Soko la Minada na Soko la Awali

Kiasi cha korosho ghafi zilizouzwa kupitia Soko la Minada ni tani 409,038.599 zenye thamani ya shilingi 1,469,036,244,102.2 ambapo daraja la kwanza ni tani 390,359.534 zenye thamani ya Shilingi 1,421,684,143,553.60 na daraja la pili tani 18,679.065 zenye thamani ya Shilingi 47,352,100,548.60. Bei ya juu kwa daraja la kwanza ni shilingi 4,195 na bei ya chini ni Shilingi 1,810 na daraja la pili bei ya juu ni shilingi 2,870 na bei ya

chini Shilingi 1,410. Bei ya wastani kwa daraja la kwanza ilikuwa shilingi 3,592 na daraja la pili shilingi 2,140 kwa kilo. Kwa upande wa Soko la Awali mauzo ni tani 10,029.281 zenye thamani ya shilingi 25,073,202,500. Mauzo ya korosho ghafi katika Soko la Awali kwa ajili ya kubangua ndani ya nchi ziliuzwa kati ya 80 shilingi 3,000 hadi 2,000 ambapo wabanguaji walinunua korosho kupitia AMCOS na wengine waliingia mnadani na kununua korosho kwa njia ya ushindani. Wakulima walilipwa fedha zao kupitia akaunti zao, makato mengine ambayo ni ushuru wa Halmashauri, ushuru wa chama kikuu, magunia na tozo nyingine zililipwa na mnunuzi.



*Wakulima wa Chama Kikuu cha Ushirika cha TANECU wakifuatilia mauzo ya korosho zao kupitia TMX msimu wa 2024/2025.*

### 5.1.5.2 Kusimamia na kudhibiti usafirishaji wa Korosho ghafi na karanga ndani na nje ya nchi ili kuimarisha mfumo wa mauzo kupitia Stakabadhi za ghala, Soko la Awali na mauzo ya korosho karanga.

Bodi ya Korosho kwa kushirikiana na Halmashauri imeendelea kufanya ukaguzi kupitia vizuizi ili kudhibiti usafirishaji kinyume na utaratibu. Jumla ya vibali 192 vya kusafirisha korosho nje ya nchi vimetolewa ambapo vibali 106 vya korosho ghafi na vibali 86 vya korosho karanga. Pia vibali 515 vya korosho ghafi na 1,500 vya korosho karanga vimetolewa kwa ajili ya kusafirisha korosho ndani ya nchi, shughuli hii ni endelevu.

### 5.1.5.3 Kukusanya takwimu za korosho ghafi zilizobaki kwa wakulima ili kujumuishwa kwenye takwimu za uzalishaji wa korosho ghafi kitaifa

Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele na Mamlaka za Serikali ya Mitaa na Vyama Vikuu vya Ushirika imefanya utafiti wa kubaini kiasi cha korosho ghafi zilizobaki majumbani kwa ajili ya kujumuishwa kwenye takwimu za mwisho za

uzalishaji wa korosho ghafi Kitaifa kwa msimu wa 2024/2025. Kwa mujibu wa utafiti huo korosho ghafi zilizouzwa kupitia mifumo rasmi (TMX, Soko la Awali na Wabanguaji wadogo) ni tani 452,238.704 na zilizobaki majumbani kwa ajili ya matumizi mbalimbali ni tani 76,025.116. Hivyo, takwimu ya mwisho ya uzalishaji wa korosho ghafi Kitaifa kwa msimu wa 2024/2025 ni tani 528,263.820 sawa na ongezeko la asilimia 70% ikilinganishwa na uzalishaji wa korosho ghafi msimu wa 2023/2024 ambapo iliishia tani 310,787.17.

**5.1.5.4 Ufuatiliaji wa mwenendo wa bei za Korosho ghafi nje ya nchi na usambazaji na taarifa kwa wadau mbalimbali**

Bodi imeendelea kusambaza taarifa za hali ya soko la ndani na nje ya nchi kupitia jarida maalum (Jarida la Korosho) ambalo hutolewa kila mwisho wa mwezi. Aidha Jarida hili ni endelevu na hutolewa kwa kuzingatia kalenda ya zao ndani na nje ya nchi.

**5.1.5.5 Kushiriki Mikutano na majukwaa ya kimataifa ndani na nje ya nchi.**

Bodi ya Korosho Tanzania imeendelea kushiriki majukwaa mbalimbali pamoja na kuhudhuria mikutano ya kimataifa. Kupitia mikutano hii wakulima wameunganishwa na masoko ya uhakika kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika pamoja na wabanguaji wa ndani.



*Viongozi wa Bodi ya korosho walioshiriki kwenye mkutano wa dunia wa korosho Dubai wakiwa katika ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Abu Dhabi katika umoja wa Falme za Kiarabu (UAE)*

Utekelezaji wa shughuli hizi umefanikisha uzalishaji wa korosho ghafi kufikia tani 528,263.82 ni sawa na ongezeko la asilimia 70 ukilinganisha na uzalishaji wa tani 310,787.17 za msimu 2023/2024. Vile vile uzalishaji huu ni sawa na asilimia 88.78 ya makadirio ya kuzalisha tani 595,000 kwa msimu wa mwaka 2024/2025. Pia, umeongeza ubanguaji wa korosho kufikia tani 122,578.06 kutoka tani 69,604.93 za msimu wa 2023/2024.

Hali ya ubora wa korosho ghafi umeendelea kuimarika kwa asilimia 95.4. Hii ilitokana na hatua zilizochukuliwa na Bodi ya Korosho Tanzania kusimamia na kufuatilia ubora wa korosho kuanzia ngazi ya AMCOS, ghala kuu hadi Bandari/viwandani. Aidha, korosho ghafi zimeuzwa kwa bei ya juu ya Tsh 4,195 ikilinganishwa na bei ya Tsh 2,190 kwa msimu wa mwaka 2023/2024.

## 5.2 MIPANGO YA UTEKELEZAJI YA MSIMU WA MWAKA 2025/2026

Katika msimu wa mwaka 2025/2026 malengo yaliyopo ni kuzalisha korosho ghafi tani 700,000, kuhakikisha asilimia 60 ya korosho zitakazozalishwa zinabanguliwa ndani ya nchi na kuendelea kutafuta masoko ya uhakika na endelevu ya korosho na bidhaa zake ndani na nje nchi ili mkulima na wadau wengine waendelee kupata faida kutoka kwenye zao la korosho. Hivyo, ili kufikia malengo hayo Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na wadau katika mnyororo wa thamani wa zao la korosho nchini inatekeleza mipango ifuatayo:

### 5.2.1 KILIMO

#### 5.2.1.1 Kuratibu usambazaji na ugawaji wa Pembejeo

Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) na TARI Naliendele itaendelea kuratibu usambazaji na ugawaji wa pembejeo za ruzuku za zao la korosho kwa wakulima. Lengo katika msimu wa 2025/2026 ni kusambaza sulphur tani 40,000 na Viuatilifu vya Maji Lita 3,000,000. Aidha, hadi tarehe 15 Aprili, 2025 kulikuwa na sulphur tani 44,077 na viuatilifu vya maji lita 1,474,123. Mapokezi ya viuatilifu vya maji yanaendelea.



*Mmoja wa wakulima wa korosho wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, mara baada ya kupokea pembejeo za ruzuku msimu wa 2024/2025.*

#### 5.2.1.2 Mbegu/Miche bora ya mikorosho

Kuanzia msimu wa 2025/2026 Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na TARI Naliendele imepanga kurejesha mpango wa uzalishaji wa miche bora ya mikorosho kupitia vikundi na taasisi zilizopo kwenye Halmashauri zinazolima korosho nchini ili kuongeza ufanisi wa usambazaji na ugawaji kwa wakulima. Lengo katika msimu wa 2025/2026 ni kuzalisha na kusambaza miche 10,000,000.

#### 5.2.1.3 Huduma za ugani kwa wakulima

Kupitia programu ya Jenga Kesho Iliyobora (BBT) iliyopo Wizara ya Kilimo jumla ya **Maafisa Kilimo 500** wamesambazwa na Bodi ya Korosho Tanzania katika Kata zenye fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji wa korosho ghafi kutoka Mikoa ya Mtwara (245), Lindi (152), Ruvuma (50), Pwani (29) na Tanga (24). Maafisa kilimo hao ambao ni wahitimu kutoka vyuo vya kilimo vilivyopo nchini wamepatiwa mafunzo ya kilimo bora cha zao la korosho na vitendea kazi ikiwemo pikipiki 500 na vishikwambi 500. Mafunzo hayo rejea na vifaa hivyo ni maalum kwa ajili ya kuwafikia na kuwahudumia wakulima kwa kuwasajili na kuwapatia huduma za ugani ikiwa ni pamoja na kusimamia na kufuatilia zoezi la usambazaji na ugawaji wa viuatilifu vya ruzuku kwa wakulima.



*Mkuu wa wilaya ya Tandahimba mkoani Mtwara, Kanali Michael Mtenjele akizindua ugawaji pikipiki na vishikwambi kwa maafisa kilimo wa BBT-KOROSHO ili kurahisisha shughuli za ugani kwa wakulima.*

### 5.2.2 UBANGUAJI

#### 5.2.2.1 Ujenzi wa kongani la viwanda katika Kijiji cha Maranje Mkoa wa Mtwara

Kazi zitakazotekelezwa ni kukamilisha ujenzi wa ghala mbili zenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 kila moja. kukamilisha ujenzi wa barabara ya kilomita 7.5, kujenga fensi yenye urefu wa kilomita 11, kujenga kiwanda chenye uwezo wa kubangua tani 30,000 za korosho ghafi kwa mwaka, kujenga kituo cha afya, kuweka mkuza kwenye eneo la ekari 1208 na kukamilisha majadiliano na taratibu za kisheria na wawekezaji ili kuanza ujenzi wa viwanda vingine vya kubangua korosho.

#### 5.2.2.2 Mafunzo ya kanuni bora za ubanguaji wa korosho

Mafunzo haya yatatolewa kwenye Halmashauri mbalimbali zinazolima korosho hapa nchini. Lengo ni kufikia washiriki 250 katika msimu wa 2025/2026 ili waweze kuongeza thamani ya zao kabla ya kuuza. Aidha, mafunzo ya umahiri kwenye zao la korosho (MTP 20) yatafanyika kwa awamu ya pili mwezi Juni 2025 mkoani Mtwara na awamu ya tatu mwezi Septemba 2025 nchini Kenya.

#### 5.2.2.3 Kuhamasisha uwekezaji kwenye viwanda vya kubangua korosho

Uhamasishaji huu utafanyika kupitia makongamano mbalimbali ya uwekezaji na biashara ndani na nje ya nchi ikiwemo Mkutano wa 19 wa Mwaka wa Jukwaa la Korosho Afrika ***(African Cashew Allance – ACA)*** utakaofanyika tarehe 18 – 22 Novemba 2025 Katika ukumbi wa JNICC Jijini Dar es Salaam. Hii itasadia kupata wawekezaji wa kutosha kwenye kongani la viwanda Maranje.

**5.2.2.4 Kujenga ghala la kuhifadhi korosho ghafi tani 10,000 Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru**

Bodi ya Korosho itaendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa ghala la kuhifadhia korosho ghafi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru.

**5.2.3 UDHIBITI UBORA**

**5.2.3.1 Kutoa mafunzo ya udhibiti ubora wa korosho ghafi kwa wakulima, viongozi wa Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) na wataalam katika ghala za minada**

Msimu 2025/2026 Bodi imejipanga kutoa mafunzo ya udhibiti ubora kwa wakulima zaidi 200,000, viongozi wa AMCOS zote zinazolima korosho nchini, mameneja na wataalam 150 katika ngazi ya ghala la mnada.

**5.2.3.2 Kusajili ghala zote zitakazotumika kuhifadhi Korosho**

Kupitia Sheria na. 18 ya mwaka 2009 ya Bodi ya Korosho Tanzania kifungu cha 12 (1) pamoja na kifungu cha 15 (1) na (4) vinaipa mamlaka Bodi kusajili na kutoa leseni kwa ghala zinazotumika kuhifadhi korosho. Aidha, vingi hivi vinaitaka Bodi kusajili na kutoa leseni kwa waendesha ghala kwa mujibu wa sheria hii. Katika kutekeleza sheria hii Serikali itapata faida zifuatazo:

i. Kutambua hali ya ghala na uwezo wake katika kuhifadhi korosho

ii. Kutambua waendesha ghala wenye uwezo wa kuendesha ghala pamoja na kuwasimamia

iii. Kudhibiti vitendo vya kuharibu ubora wa korosho

iv. Kudhibiti waendesha ghala wanaotoa taarifa za uongo za mchanganuo wa mauzo ya korosho kwa wanunuzi

v. Kuainisha na kutambua idadi ya ghala zinazoweza kutumika kuhifadhi korosho.

**5.2.3.3 Kufanya ukaguzi wa kawaida na kushtukiza katika ghala za Vyama vya Msingi na ghala za minada kabla na wakati wa msimu.**

Bodi itaendelea kufanya ukaguzi msimu 2024/2025 katika ghala za mnada kabla na wakati wa msimu ili kukagua uwepo na matumizi sahihi ya vifaa vya ubora vilivyohakikiwa na mamlaka husika, kukagua kama taratibu za mapokezi, uhifadhi na utoaji wa korosho kwa mujibu wa Mwongozo wa Udhibiti Ubora zinafuatwa. Aidha

ukaguzi hufanyika kuangalia uwepo wa wataalam wa ubora wenye sifa na vifaa vya kiulinzi kama vile camera.

#### 5.2.3.4 Kuimarisha usimamizi kwenye ghala za Minada

Bodi ya Korosho Tanzania msimu 2025/2026 itaimarisha usimamizi wa korosho ghala za mnada kwa kuweka wataalam katika kila ghala la mnada kusimamia mapokezi, uhakiki ubora uhifadhi na utoaji wa korosho. Aidha wataalam watatatua migogoro yote itakayojitokeza wakati wa msimu na kutoa elimu kwa Vyama vya msingi vitakavyokuwa na changamoto za ubora. Hii itahimarisha ubora na kuongeza bei ya korosho sokoni.

i. Ubora wa korosho ghafi ghalani utaimarika na kuvutia wanunuzi

ii. Bei ya korosho ghafi kwa mkulima itaongezeka kwasababu ya ubora wa korosho ghalani

iii. Mapato ya serikali yataongezeka kutokana na tozo za korosho kutoka kwa wanunuzi

iv. Hakutakuwepo kwa vitendo vya hujuma za biashara haramu ya korosho ghalani

v. Kila taasisi inayohusika katika kupokea na kuhifadhi korosho ghalani itasimamiwa kikamilifu kwa kuzingatia sheria hii.

### 5.2.4 MASOKO

#### 5.2.4.1 Kusajili magari yote yatakayotumiwa kusafirisha korosho

Kutokana na changamoto ya baadhi ya watu kuhujumu biashara ya korosho kwa kubadilisha korosho safi na bora za wanunuzi na vitu vichafu vinavyofanana na korosho wakati wa usafrishaji kuelekea bandarini wakati wa msimu, Bodi ya Korosho Tanzania kwa kutumia Sheria na. 18 ya mwaka 2009 kupitia Kifungu cha 5 (2) (b) na (e) kinatoa mamlaka kusajili makampuni ya usafirishaji pamoja na magari yatakayotumika kusafirisha korosho. Lengo ni kuzuia na kudhibiti hujuma ambazo zinailetea hasara serikali na kuingiza nchi katika migogoro ya kidpromasia ya kiuchumi, Kwa kusimamia eneo hili serikali itapata faidha zifuatazo:

i. Bei ya korosho itaongezeka kwani wanunuzi watapa Imani na usalama wa biashara zao.

ii. Hakutakuwa na migogoro ya biashara baina ya wanunuzi na seriakali Pamoja na mahusiano ya Tanzania na nchi zinazonunua korosho ya Tanzania yataimarika.

iii. Utoroshwaji wa korosho bila vipari kupitia magari yasiyotambulika utadhibitiwa.

iv. Kampuni ya usafirishaji itawajibika kumlipa mnunuzi korosho zake zitakazobadilishwa na vitu vichafu kwasababu atakuwa anatambuliwa na mamlaka baada ya kusajiliwa.

v. Serikali itaongeza mapato kupitia kodi mbalimbali katika mnyororo wa shughuli za usafirishaji kutokana na mapato yatakayopatikana kutoka kwa makampuni yaliyosajiliwa na Bodi.

**5.2.4.2 Kusajili mikataba itakayoingiwa kati ya mnunuzi na muuzaji wa zao la korosho nchini.**

Kumekuwepo na kesi nyingi za wanunuzi wa korosho karanga kudhurumiwa korosho zao baada ya kufanya malipo. Baadhi ya kampuni za wauzaji ambayo ni ya kitanzania wamekuwa wakiingia mikataba ya kuuziana korosho wakati wengi hata hawana leseni na hawafanyi biashara ya korosho. Wanunuzi ambao wamekuwa wakidhurumiwa ni wa kigeni hasa kutoka katika nchi za Uturuki, Lebabon na Jordan. Katika jukumu hili Kifungu cha 15 (1) na (4). Hatua hii ipo kisheria na inalenga kudhibiti vitendo hivi na kulinda masrahi ya mnunuzi.

**5.2.4.3 Kusimamia mifumo na utoaji wa leseni mbalimbali za korosho**

Hii itasaidia serikali kurahisisha kutoa huduma kwa wahitaji wa leseni na kupata takwimu za kiasi cha korosho kilichouzwa na kutambua wahusika wa biashara hiyo

**5.2.4.4 Kudhibiti upotevu wa korosho ghalani**

Bodi itahakikisha korosho zilizonunuliwa na mnunuzi zinakuwepo ghalani kama hati (*catalogue*) ya mauzo inavyoonesha. Kila ghala kutakuwa na msimamizi ambaye atahakikisha kila mwendesha ghala ana leseni ya uendeshaji ya WRRB, ana leseni ya CBT na ghala husika limesajiliwa na CBT. Hii ni kwa mujibu wa Kifungu cha 12 (1) na Kifungu cha 15 (1) na (4).

**5.2.4.5 Kusajili wanunuzi na kuhakikisha wanalipia bondi kabla ya kuunganishwa na mtandao wa TMX kushiriki minada**

Hili ni jukumu muhimu la usajili wa wanunuzi ambao watashiriki kununua korosho minadani. Bila kusajiliwa wanunuzi hawawezi kushiriki na wala kuunganishwa na mfumo wa kidigitali wa TMX. Kupitia usajili huu serikali inapata uhakika wa wanunuzi na pesa ya mauzo ya korosho ya wakulima inakuwa na uhakika wa kupatikana kutokana na uwepo wa dhamana kwa njia ya bondi.

**5.2.4.6 Kuainisha masoko mapya na kuuwaunganisha wanunuzi kwa wakulima kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika na wabanguaji wa ndani**

Bodi itaendelea kushiriki mikutano na majukwaa ya ndani na ya kimataifa kwa ajili ya kutafuta masoko yenye uhakika na kuhamasisha uwekezaji katika tasnia ya korosho nchini. Kupitia shughuli hii serikali itakuwa imefanikiwa kuongeza wigo wa soko la korosho kwa kuongeza mauzo ya korosho nje ya nchi ili kupata fedha za kigeni.

**5.2.4.7 Kusimamia uendeshaji wa Korosho Marathon katika tasnia ya korosho nchini**

Hii ni moja ya mbio za hisani inayofanyika kila mwaka kama sehemu ya mkakati wa kukuza soko la korosho kwa kuhamasisha ulaji wa korosho, matumizi ya mazao ya korosho na kuongeza usindikaji. Vile vile sambamba na kufanya mbio utanguliwa na wiki ya maonesho ya bidhaa mbalimbali kutoka kwa wadau na wadau kama TRA,

Taasisi za kifedha kama CRDB, TADB na NMB utumia wiki ya maonesho kutoa elimu kwa wakulima pamoja na washiriki wengine.




*Washiriki wa awamu ya tatu ya mbio za Korosho Marathon ambazo kilele chake kilikuwa katika viwanja vya Milleneum beach mkoani Mtwara oktoba 26, 2024.*

**AGENDA NA. 6: KUPOKEA TAARIFA YA MAENDELEO YA UTAFITI KATIKA ZAO LA KOROSHO**

## TAARIFA YA MAENDELEO YA UTAFITI KATIKA ZAO LA KOROSHO

### 6.1 Utangulizi

Korosho ni miongoni mwa mazao 13 ya kimkakati nchini Tanzania, na ni zao kuu la kibiashara linalochangia pato la wakulima na taifa kwa ujumla. Zao hili limeendelea kuwa la muhimu na kulimwa kwa wingi nje na ndani ya nchi yetu. Hii ni kutokana na sababu kuwa uhitaji wa korosho katika soko la ndani Pamoja na nje ya Tanzania umeendelea kuwa mkubwa.

Pamoja na umuhimu wa zao hili la korosho nchini, bado zipo changamoto mbali mbali zinazowakabili wakulima na wadau mbalimbali katika mnyororo mzima wa zao hili kuanzia uzalishaji mpaka uongezaji wa thamani. Hivyo, ili kutatua changamoto hizo Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) kituo cha Naliendele, kina jukumu la kufanya utafiti kwenye zao la Korosho ili kutatua changamoto zinazowakabili wakulima na wadau wa korosho.

TARI kupitia kituo cha Naliendele pamoja na majukumu mengine ina jukumu la kufanya utafiti kwenye zao la korosho kama ifuatavyo:

(i) Kugundua na kuzalisha mbegu bora za korosho
(ii) Kubaini na kupendekeza njia bora za uzalishaji miche ya korosho
(iii) Kuanzisha mashamba ya kuzalishia vikonyo kwaajili ya kubebeshea miche
(iv) Kubaini na kupendekeza maeneo yanayofaa kwa kilimo cha korosho
(v) Kutafiti teknolojia za kilimo bora cha korosho na kupendekeza kwa wakulima
(vi) Kubaini mbinu za kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa korosho
(vii) Kugundua viuatilifu hai vya kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa korosho
(viii) Kubaini wadudu rafiki wa zao la korosho na namna ya kuwatumia
(ix) Kubaini mbinu za kuboresha na kufufua mashamba ya korosho yaliyotelekezwa
(x) Kubaini na kutumia mbinu za bayoteknolojia katika kuzalisha mbegu bora za korosho
(xi) Kufanya utafiti wa udongo na matumizi bora ya ardhi kwenye zao la korosho

(xii) Kutafiti mbinu za uongezaji thamani korosho na mabibo

(xiii) Kutoa elimu kwa maafisa ugani juu ya teknolojia zilizopendekezwa katika kilimo cha zao la Korosho

**Uzalishaji wa mbegu na miche bora za korosho**

Uzalishaji wa mbegu na miche bora ya korosho inazalishwa na kituo cha TARI Naliendele na vituo vidogo vilivyo chini ya TARI Naliendele. Vituo hivyo vijulikanavyo kama vituo vya uendelezaji zao la korosho yaani 'Cashewnuts Development Centres, CDCs), ambavyo ni:- Nyangao (Lindi Vijijini), Nanyanga (Tandahimba), Nakayaya (Tunduru), Mkuranga (Mkuranga), Mkumba (Nachingwea), Mtopwa (Newala) na Chambezi (Bagamoyo). Vituo hivi vilianzishwa karibu na wakulima kwenye mikoa inayolima korosho ambayo ni Mtwara, Lindi, Pwani, Tanga na Ruvuma. Pia mashamba ya kuzalishia mbegu za korosho yameongezwa katika maeneo ya Lusewa na Paradiso mkoani Ruvuma, Manyoni Mkoa wa Singida,Tumbi katika mkoa wa Tabora, Pangani na Mkinga katika mkoa wa Tanga. Kupitia vituo hivi tumeendelea kutoa huduma mbalimbali ambapo wadau wanaozunguka maeneo husika huweza kutembelea vituoni na kupata elimu ya kanuni za kilimo bora cha zao la korosho.

Aidha, ili kuhakikisha wakulima wanapata huduma kwa urahisi ikiwemo upatikanaji wa mbegu bora, miche na elimu ya kanuni bora za kilimo cha korosho, TARI Naliendele imeanza kujengea uwezo mtaalam mmoja mmoja kutoka katika vituo vya TARI Tumbi, TARI Makutupora na TARI Mikocheni ili waweze kusaidia kutoa huduma ya kilimo bora cha korosho kwenye mashamba/ vituo vya uendelezaji wa zao la korosho kwakuwa vituo hivi vya TARI viko jirani na mashamba ya korosho ya TARI Naliendele.

### 6.2 Kazi za program ya korosho zilizofanyika katika mwaka wa Fedha 2023/2024

| Na | KAZI | MAFANIKIO | KAZI ZINAZOENDELEA |
|---|---|---|---|
| 1 | Uzalishaji wa mbegu bora za korosho | Uzalishaji wa mbegu umeongezeka na kufikia tani 59 katika msimu wa 2024/2025 ukilinganisha na tani 30.38 kwa msimu wa 2023/2024. Ongezeka hili la uzalishaji wa mbegu ni sawa na asilimia 194.2. | Uzalishaji wa mbegu bora za korosho unaendelea kwa msimu wa 2025/2026. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2 | Uzalishaji miche ya zao la korosho | Kwa msimu huu 2024/2025 uzalishaji wa miche umeongezeka hadi kufikia miche 1,350,000 ukilinganisha na miche 318,928 kwa msimu wa mwaka 2023/2024. Ongezeka hili la uzalishaji wa miche ni sawa na asilimia 423.2. Aidha uzalishaji wa miche iliyobebeshwa yenye ukinzani na ugonjwa wa blaiti unaendelea hadi sasa tumeshabebesha miche 500,000 na miche itaanza kupatikana mapema mwanzoni mwa msimu wa 2025/2026 | Uzalishaji wa miche utaendelea kulingana na mahitaji ya wakulima |
| 3 | Uanzishwaji na uendelezaji wa Mashamba ya mbegu bora za korosho | Jumla ya ekari 40 zaidi za Mashamba mapya ya kuzalisha mbegu bora za korosho yameongezwa katika eneo la Nyangao, Lindi na sasa kufikia jumla ya ekari 403 ya mashamba ya mbegu bora za korosho. | Mashamba tayari yanazalisha mbegu na yanaendelea kuhudumiwa |
| 4 | Uanzishaji wa Mashamba ya vikonyo vya mbegu mpya 8 | Jumla ya ekari 16 zenye mikorosho 432 zimebebeshwa kwa ajili ya kuzalisha vikonyo vya kuzalishia miche ya mbegu mpya kama ifuatavyo;- Naliendele ekari 4.5, Mtopwa 2, Nanyanga 2.5, Nachingwea ekari 5 na Tunduru ekari 2 | Kuendelea kuhudumia mashamba haya ili yazalishe vikonyo kwa ajili ya kubebesha miche yenye ukinzani na blaiti. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5 | Ugunduzi wa mbegu bora za korosho dhidi ya ugonjwa wa blaiti | Taasisi imefanikiwa kugundua aina mpya nane (8) za zao la korosho zenye ukinzani na ugonjwa wa blaiti. Aina hizo za Mbegu ni TARIKO 1, TARIKO 2, TARIKO 3, TARIKO 4, TARIKO 5, TARIKO 6, TARIKO 7 na TARIKO 8. Ugunduzi huu, utasaidia kupunguza matumizi ya Viuatilifu vya magonjwa. | Kuendelea kutunza mikorosho mama ya aina hizi 8 |
| 6 | Utafiti wa aina 18 za mbegu zinazozaa mapema zinaemdelea kufanyiwa utafiti | Huu ni mwaka wa 5 na takwimu zinaonesha kati ya aina 18 aina tano (5) zinazaa mapema. | Kuendelea na uchunguzi wa mbegu hizi katika mashamba ya wakulima kwa mazingira tofauti |
| 7 | Aina 35 za mbegu za korosho kwa ajili ya Uzalishaji wa mabibo | Huu ni mwaka wa tano, utafiti unaendelea na takwimu zinaendelea kuchukuliwa. | Kuendelea na utafiti pamoja na kuchukua takwimu |
| 8 | Kufanya Utafiti wa Mbolea kwenye korosho | Matokeo ya awali yameonesha mbolea za kwenye majani, aina tatu zinafanya vizuri. Aidha taasisi inafanya uidhinishaji wa ufanisi wa mbolea hizo. Na matokeo ya ufanisi huu yatakuwa tayari musimu wa 2025/2026 | Utafiti unaendelea ili kuthibitisha na kuidhinisha ufanisi wa aina tatu za Mbolea zilizopendekezwa awali |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9 | Mbinu za kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu | ➢ Taasisi imefanikiwa kupanua wigo wa Viambata Amilifu; ambapo viuakuvu aina ya *azoxystrobin, carbendazim na propamorcarb hydrochloride* vimeongezeka kwa ajili ya Magonjwa (Blaiti na Ubwiriunga), na;<br>Viuadudu *aina ya Abamectin, emamectin benzoate, Imidaclopid, Imidaclopin,* vimeongezeka kwa ajili ya wadudu waharibifu wa korosho.<br>➢ Viuakuvu vya asili vya Wadudu aina ya Pyrethrin vinavyotokana na Pareto, vimeonesha ufanisi mzuri wa awali kwenye kudhibiti Wadudu wa mikorosho, matokeo haya yatasaidia kupunguza matumizi ya Viuati kikemikali. | ➢ Kufanya utambuzi wa visumbufu vipya na kufuatilia maendeleo ya visumbufu vya zamani katika misimu ya korosho.<br><br>➢ Kuthibitisha na kuidhinisha mbinu za kibaiolojia ikiwemo viuakuvu vya kibaiolojia *(biopesticide)*. Pia biolojia-mimea *(botanical pesticides) unaendelea* |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 10 | Utafiti wa ugonjwa wa Mnyauko fusari | Taasisi imefanikiwa kuthibitisha mbinu mbili ambazo zimeweza kudhibiti ugonjwa wa Mnyauko Fusari; nazo ni<br>a. Matumizi ya viuakuvu vya kibaiolojia jamii ya *Bacillus spp.,* na *Trichoderma sp.,* vimefanikiwa kukinga mikorosho kabla ya kushambuliwa.<br>b. Matumizi ya Viuakuvu vya kemikali jamii ya Carbendazim, Azoxystrobin, Thiophanate methyl na Propamorcarb hydrochloride vikiambatana na mbinu ya ubebeshaji wa mikorosho ilioathirika. | ➢ Kuendelea na program ya kudhibiti ugonjwa wa Mnyauko Fusari katika mashamba ya korosho.<br>➢ Kutoa elimu kwa wakulima juu ya matumizi ya njia za kudhibiti ugonjwa wa mnyauko fusari. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11 | Uongezaji thamani wa korosho na mabibo | ➢ Thamani ya bibo imeongezwa na kuzalisha "*Ethanol*" na nyama ya mabibo<br><br>➢ Utafiti wa awali wa aina mbili za "*Mbolea ya mabibo*" ikiwemo; Mbolea ya maji na Mbolea ya unga unaendelea.<br><br>➢ Thamani ya korosho imeongezwa kwa kuzalisha "maziwa", Siagi, na unga wa korosho | ➢ Kuendelea kuongeza thamani ya bibo ili kupandisha kiwango cha ethanol mpaka angalau asilimia 95. Aidha Ujenzi wa kiwanda chenye uwezo wa kutafiti na kuzalisha ethanol unahitajika.<br><br>➢ Kuendeleza utafiti lengo ni kupata mbolea hai inayotokana na mabibo<br><br>➢ Kuboresha kiwanda cha Utafiti na ubanguaji wa korosho. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 12 | Kutoa elimu ya kilimo bora cha zao la korosho kwa kushirikiana na wadau mbalimbali | - Jumla ya Maafisa ugani 928 kati ya hao 395 ni kupitia BBT wamepewa elimu juu ya kilimo bora cha zao la korosho<br>- Teknolojia ya ufufuaji wa mashamba pori imetolewa kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya kwa mikoa ya Mtwara na Pwani; ambapo mashamba 19 yamefufuliwa mkoa wa Mtwara na 6 mkoa wa Pwani.<br><br>Teknolojia ya utunzaji wa mashamba na udhibiti wa visumbufu zimetolewa kwa kuanzisha mashamba 32 ya mfano (Demonstration Plots): ambapo 8 kutoka Lindi, 15 Mtwara, 3 Ruvuma na 6 Pwani | Kuendelea kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali kwa njia ya mafunzo ya ana kwa ana, mashamba ya mfano/darasa, na vyombo vya habari |

## 6. 3. Changamoto

### 6.3.1. Mabadiliko ya Hali ya Hewa

Kituo kimeendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwenye zao la korosho. Kuongezeka kwa siku za mvua katika kipindi cha uzalishaji wa korosho kumeonekana.

**Jedwali Na. 8:** Hali ya mazingira ya mvua na unyevu kwenye misimu ya Uzalishaji wa korosho.

| **Hali ya hewa** | **Mwezi (Juni-Septemba)** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
| Mvua za nje ya msimu (mm) | 21.18 | 30.94 | 39.02 | 42.1 |
| Unyevu angani (%) | 67 | 70 | 73 | 70.3 |
| Jumla ya siku za mvua | 4 | 8 | 12 | 11 |

#### 6.3.2. Milipuko ya Magonjwa

Kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, kumekuwa na milipuko ya magonjwa na wadudu waharibifu ndani ya msimu wa uzalishaji wa korosho katika maeneo mbalimbali. Magonjwa kama vile blaiti, ubwiriunga, vithiripi na ugonjwa wa chule huwa ni changamoto kwenye zao la korosho hasa usipodhibiti.

### 6.4. Kazi zinazoendelea ni Pamoja na:

i. Kuendelea kutunza mashamba ya mbegu
ii. Kuendelea kuzalisha miche bora ya mikorosho
iii. Kuendeleza mashamba ya vikonyo ikiwemo mashamba ya vikonyo vya mbegu bora 8 zilizosajiliwa mwaka jana
iv. Kuendeleza Utafiti wa aina 35 kwa ajili ya uzalishaji wa mabibo
v. Kuendeleza Utafiti wa aina18 za korosho zinazozaa mapema (early yielding)
vi. Utafiti unaendelea ili kuthibitisha na kuidhinisha ufanisi wa aina tatu za Mbolea zinazoonesha kufanya vizuri kutokana na matokeo ya awali
vii. Kufanya utambuzi wa visumbufu vipya na kufuatilia maendeleo ya visumbufu vya zamani katika misimu ya korosho
viii. Kufanya utambuzi wa visumbufu vipya na kufuatilia maendeleo ya visumbufu vya zamani katika misimu ya korosho.
*ix.* Kuthibitisha na kuidhinisha mbinu za kibaiolojia ikiwemo viuakuvu vya kibaiolojia *(biopesticide)*. Pia biolojia-mimea *(botanical pesticides) unaendelea*
x. Kuendelea na program ya kudhibiti ugonjwa wa Mnyauko Fusari katika mashamba ya korosho.
xi. Kufanya ugunduzi wa mashine rahisi ya kutenganisha bibo na korosho karanga
xii. Kutoa elimu kwa maafisa ugani juu juu ya kilimo bora cha zao la korosho

### 6.5. Utekelezaji wa Miradi miwili (2) inayofadhiliwa na European Union (EU) kwa kushirikiana na BMZ Ujerumani kupitia GIZ

TARI Kituo cha Naliendele itaanza kutekeleza miradi miwili (2) kwenye zao la korosho kama ifuatavyo:

**Mradi 1: '***Development of Climate Resilient Pests and Diseases Management Strategies for Improving Livelihood Standards of Cashew Growers in Tanzania and Mozambique'*

Mradi huu una malengo mahususi kama ifuatavyo;

(i) Kufanya utafiti zaidi kwenye visumbufu vya wadudu na magonjwa
(ii) Kupata kiuatilifu hai kwa ajili ya kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa korosho
(iii) Kuwa na teknolojia ya kumwezesha mkulima kutambua visumbufu na mbinu za kutatua changamoto hizo kwa kutumia simu ya mkononi
(iv) Kutoa elimu kwa maafisa ugani angalau 1000 namna ya kutumia teknolojia ya simu katika kutambua magonjwa na wadudu waharibifu kwenye zao la korosho

**Mradi wa 2 '***Enhancing the Utilization of Cashew Apple for Climate Resilient, Increased Income and Food Security of Smallholder Farmers in Tanzania and Mozambique'*

**Malengo mahususi ya mradi huu ni:**

(i) Kuzalisha mbolea hai kwa kutumia mabibo ya korosho
(ii) Kuzalisha vyakula vyenye vitamini C kutoka kwenye mabibo ya korosho
(iii) Kushirikiana na taasisi ya Utafiti ya Msumbiji katika kuongeza thamani ya mabibo kukaa kwa muda mrefu kabla ya kuyatumia kwa kazi mbali mbali

### 6.6 Mwelekeo wa Msimu wa Korosho 2025/2026

Pamoja na mvua za wastani hadi chini ya wastani zilizotabiriwa na Mamlaka ya hali ya hewa (TMA) hasa maeneo mengi yanayolima zao la korosho kwa kipindi cha Novemba/Disemba 2024 mpaka April/May 2025, bado kutakuwa na uzalishaji mzuri kwani mvua kubwa za msimu 2023/2024 bado zimefanya kiwango cha maji kuwa kizuri kwa mazao jamii ya miti ukiwemo mkorosho.

Aidha uzalishaji wa tija utategemea matumizi sahihi ya teknolojia zilizopendekezwa kama vile matumizi sahihi na salama ya viuatilifu, matumizi ya mbegu bora na kilimo bora cha korosho kwa ujumla. Pia hali ya hewa kipindi cha mwezi wa saba mpaka wa tisa ambapo uzalishaji hupendelea uwepo wa jua, unyevu kidogo angani, kuwepo na joto na kusiwe na mvua.

### 6.7 Hitimisho

TARI Kituo cha Naliendele, kinaendelea na Shughuli mbalimbali za Utafiti wa zao la korosho ili Kuongeza tija ya Uzalishaji. Pia tunashukuru kwa Serikali na wadau wetu kwa mazingira wezeshi yanayotusaidia kufanikisha utafiti kwa lengo la kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wakulima pamoja na wadau wengine katika mnyororo mzima wa zao.

## AGENDA NA. 7: TAARIFA KUTOKA MAMLAKA YA BANDARI YA MTWARA

## 7.0. TAARIFA KUTOKA MAMLAKA YA BANDARI YA MTWARA

### 7.1 Utangulizi

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alifanya ziara Mkoani Mtwara ambapo tarehe 15 Septemba, 2023 alipata fursa ya kutembelea Bandari ya Mtwara. Katika ziara hiyo Mheshimiwa Rais alielekeza kuwa, kuanzia mwaka 2023/2024 korosho zote zinazozalishwa katika Mikoa ya Kusini mwa Tanzania zisafirishwe kupitia Bandari ya Mtwara. Zoezi hilo lilitekelezwa na limeendelea kutekelezwa katika msimu wa mwaka 2024/2025 kwa mafanikio makubwa.

### 7.2 Utekelezaji wa kusafirisha shehena ya korosho kwa mwaka 2024/2025

#### 7.2.1 Upatikanaji wa Meli na Makasha

Hadi kufikia tarehe 05 Machi, 2025 Bandari ya Mtwara imehudumia jumla ya Meli **37** na kupokea Makasha Matupu **11,798** ***(Discharged)*** kutoka kampuni mbalimbali za Meli ambapo Makasha **421** yana ukubwa wa futi 20 na Makasha **11,377** yana ukubwa wa futi 40.

Aidha, jumla ya Makasha **11,638** ***(Loaded)*** yalisafirishwa kwenda nchi za nje kwa mchanganuo ufuatao; Makasha **8,126** ya ukubwa wa futi 40 na Makasha **216** ya ukubwa wa futi 20 yalisarifishwa kwenda nchini India na Makasha **1,816** ya ukubwa wa futi 40 na Makasha **23** ya futi 20 yalisarifishwa kwenda nchini Vietnam. Jumla ya Makasha **1,232** ya futi 40 na **223** ya futi 20 yalisafirishwa yakiwa matupu bila ya shehena ya korosho.

Hadi kumalizika kwa msimu wa korosho kwa mwaka 2024/2025, Bandari ya Mtwara imefanikiwa kuhudumia jumla ya Makasha **23,436** na kusafirisha jumla ya **Tani 370,896** za korosho**.**

### 7.3 Changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji

Katika kutekeleza zoezi la usafirishaji wa korosho kupitia Bandari ya Mtwara, changamoto zifuatazo zilijitokeza:

i Upungufu wa baadhi ya mitambo ikiwemo *Reachstackers, Empty Handlers na Terminal Tractors.*

ii Ufinyu wa eneo la kufungashia korosho (*Stuffing*) wakati wa zoezi la usafirishaji wa korosho kutokana na wingi wa makasha.

iii Mvua kubwa zilizosababisha kupungua kwa kasi kwa baadhi ya shughuli za utekelezaji.

**7.4 Hatua za utatuzi wa changamoto**

i. Baada ya Mamlaka kuongeza idadi ya mitambo miwili ya kushusha na kupakia shehena kwenye meli (*Mobile Harbor Cranes* za Tani 63 na 100). Mamlaka imeongeza mitambo mingine mitatu ya kuhudumia shehena *(Empty handler 1 na Wheel loaders 2)* vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi Bilioni 1.5

ii. Mamlaka inaendelea kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya ununuzi wa mitambo zaidi ili kwenda sambamba na ukuaji wa Bandari ya Mtwara katika kuhudumia shehena. Kwa sasa Mamlaka inaendelea na zoezi la kusimika mtambo mpya wa kisasa wa kuhudumia Makasha (SSG) wenye thamani ya takriban Shilingi Bilioni 52.5 ambapo zoezi hilo limeanza kutekelezwa tangu mwezi Februari, 2025.

iii. Bandari ya Mtwara inaendelea na zoezi la kuboresha maeneo ya kuhifadhia shehena. Aidha, katika msimu wa korosho wa mwaka 2024/2025, maeneo yenye jumla ya ukubwa wa mita za mraba takriban 60,000 yalitengwa na kuboreshwa kwa ajili ya kuhifadhia shehena ya Makasha.

iv. Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Kisiwa/Mgao wenye thamani ya Shilingi Bilioni 435.6 umeanza kutekelezwa kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kuhudumia shehena katika Bandari ya Mtwara. Bandari hiyo itatumika kuhudumia shehena chafu ikiwemo Makaa ya Mawe, Saruji, *Clinker* na *Sulphur* hivyo kusaidia kuongezeka kwa eneo la utekelezaji katika Bandari iliyopo sasa.

v. Bandari ya Mtwara inaendelea kuhamasisha Wadau mbalimbali kuwekeza zaidi katika miundombinu ya kufungushia shehena (CFS) ambapo kwa sasa kuna CFS mbili (2) zinazomilikiwa na Wadau wa Sekta Binafsi. Ongezeko la miundombinu hiyo litasaidia kutatua changamoto ya ufinyu wa maeneo ya kufungashia na kuhifadhia shehena Bandarini.

### 7.5 Mpango wa utekelezaji wa kusafirisha shehena ya korosho kwa mwaka 2025/2026

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania kupitia Bandari ya Mtwara imejipanga katika kuongeza ufanisi zaidi wa kuhudumia shehena msimu wa mwaka 2025/2026 kwa kutekeleza masuala yafuatayo:-

i. Kuendelea kusafirisha korosho za Mikoa ya Kusini kupitia Bandari ya Mtwara.
ii. Kuendelea na vikao vya mara kwa mara kati ya TPA na Wadau wanaohusika katika mnyororo mzima wa thamani wa biashara ya korosho ili kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza wakati wa shughuli za utekelezaji.
iii. Kuanza kufanya maandalizi ya msimu wa korosho mapema kuanzia mwezi Mei, 2025.
iv. Ifikapo mwezi Julai, 2025 Mtambo wa SSG unaoendelea kufungwa katika Bandari ya Mtwara utaanza rasmi kutumika katika kuhudumia shehena ya makasha.

### 7.6 Hitimisho

Bandari ya Mtwara imefanikiwa kutekeleza maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusafirisha korosho yote iliyowasilishwa Bandarini. Mafanikio hayo yametokana na ushirikiano mkubwa wa Watumishi wa Bandari pamoja na ushirikiano wa karibu kati ya Bandari na Wadau wote wanaohusika katika mnyororo mzima wa thamani wa zao la korosho. Ni matumaini yetu kuwa, ushirikiano huu utadumishwa na kuimarika zaidi katika msimu ujao wa mwaka 2025/2026 ili kuvuka malengo ya utekelezaji wa msimu uliopita.

**AGENDA NA. 8: TAARIFA KUTOKA BODI YA USAIMAMIZI WA STAKABADHI YA GHALA**

### 8.1.1 Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala

**WRRB** ni taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara iliyoundwa kwa Sheria Namba 10 ya 2005 na Marekebisho Kifungu **4 Sura 339 R.E. 2016** iliyopewa majukumu chini ya **Kifungu 5 (a-j)** ikiwemo kutoa leseni kwa waendesha ghala, meneja dhamana na wakaguzi wa ghala; kuchapa na kuidhinisha vitabu vya Stakabadhi za Ghala, kusajili na kuingiza taarifa za wadau muhimu wa mfumo, kuwakilisha nchi katika masuala ya taifa na kimataifa yahusuyo Mfumo wa Stakabadhi za Ghala pamoja na majukumu mengine kama taasisi itakavyoelekezwa na Mhe. Waziri wa Viwanda na Biashara.

### 8.1.2 Ghala zilizopatiwa Leseni

Katika Msimu wa Korosho Mwaka 2024/2025 Bodi ilitoa jumla ya leseni za kuendesha **Ghala Kuu 48** kwa kampuni za **Waendesha Ghala 39** zilizofanya kazi katika **mikoa 7** inayozalisha korosho ikiwemo Lindi **(15)**, Mtwara **(19)**, Pwani **(7)**, Ruvuma **(3)**, Morogoro **(2),** Singida **(1)** na Tanga **(1)** inayojumuisha **wilaya 12** kama inavyoonekana katika *Jedwali Na.9*.

**Jedwali Na.9: Ghala Kuu za Korosho 2024/2025**

| N | Ghala | Mwendesha Ghala | Mkoa | Eneo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kilwa DC. | Tanyusa Company Ltd | Lindi | Kilwa |
| 2 | Buco Lindi Cashew Nut Industries Limited | Sumajkt Logistic Company Limited | Lindi | Lindi |
| 3 | Gpsa | Demuton Tanzania Ltd | Lindi | Lindi |
| 4 | Ilulu Cooperative Union Limited | Kumahanda General Supply | Lindi | Lindi Vijijini |
| 5 | Treasury Register. | Tanyusa Company Ltd | Lindi | Lindi Vijijini |
| 6 | Hassani Yassini Mpako | Liwale Tabasamu Company Limited | Lindi | Liwale |
| 7 | Umoja Amcos Ltd. | Zuma General Trading Company Limited | Lindi | Liwale |
| 8 | Epza (Lindi Farmers Ltd) | Ahn & Raka Company Ltd | Lindi | Nachingwea |
| 9 | Export Trading Company Limited | Zuma General Trading Company Limited | Lindi | Nachingwea |
| 10 | Ibrahimu Somea Mushangani | Miki General Traders Company Ltd | Lindi | Nachingwea |
| 11 | Lijawa | Stecuria Investment Company Limited | Lindi | Nachingwea |
| 12 | Nachingwea Dc. | Lenzaq Holdings Limited | Lindi | Nachingwea |


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 13 | Shamshu Feroz. Ibrahim | The Prominence Global Traders And Co Ltd | Lindi | Nachingwea |
| 14 | Lipande-Ruangwa Dc | Ruangwa Warehousing Company Ltd | Lindi | Ruangwa |
| 15 | Runali Cooperative Union Limited | Ahn & Raka Company Ltd | Lindi | Ruangwa |
| 1 | Afrisian Ginning Ltd-Mtandi | D&B Agribusiness Co.Ltd | Mtwara | Masasi |
| 2 | Ali Mohamed Salim (Millenium). | Mtambaswala Company Limited | Mtwara | Masasi |
| 3 | Chisonga | Perfect Cashew Kernel Ltd | Mtwara | Masasi |
| 4 | Mamcu Ltd. | Mikat Agribusiness Ltd | Mtwara | Masasi |
| 5 | Masasi Dc | Mandiwa Agro Products Limited | Mtwara | Masasi |
| 6 | Micronix System Ltd - Warehouse 1&2 | Makita Agrifood Limited | Mtwara | Masasi |
| 7 | Remigio V. Naga. | Vika General Company Limited | Mtwara | Masasi |
| 8 | Olam Limited | Nampachila Business Company Limited | Mtwara | Mtwara |
| 9 | Cashewnut Company (2005) Limited | Mufena Company Limited | Mtwara | Mtwara MC |
| 10 | Mamcu Ltd Nanyamba | Mkaba General Traders Co.Limited | Mtwara | Nanyamba TC |
| 11 | Libenga Investment Ltd. | Bojomosa Agriventure Company Limited | Mtwara | Nanyumbu |
| 12 | Mamcu Ltd | Geju Investment And General Supply Company Limited | Mtwara | Nanyumbu |
| 13 | Mohamed Kossa Abdallah | Twenyuka Company Limited | Mtwara | Nanyumbu |
| 14 | Yusra Hamza. Said | Dreams On Development Company Limited | Mtwara | Nanyumbu |
| 15 | Micronix System Limited - Warehouse 1&2. | Cropstan Investment Limited | Mtwara | Newala |
| 16 | Tanecu Limited - Newala. | Ace Global Depository (T) Limited | Mtwara | Newala |
| 17 | Tanecu Limited (Agrofocus) | Sb Logistics & Company Limited | Mtwara | Newala |
| 18 | Tanecu Ltd-Chiwonga | Dreams On Development Company | Mtwara | Newala |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Limited | | |
| 19 | Tanecu Ltd - Tandahimba. | Bin Swalehe General Dealers Ltd | Mtwara | Tandahimba |
| 1 | Misugusugu Amcos Limited | Zuboma General Supplies | Pwani | Kibaha |
| 2 | Corecu (1984) Ltd - A & B | Krenk Agro (T) Ltd | Pwani | Kibiti |
| 3 | Juma Ally Ngwaya - Bungu | Pugna Agrifood Tanzania Ltd | Pwani | Kibiti |
| 4 | Kiegeani | Mafia Cashewnut & Coconut Cooperative Society | Pwani | Mafia |
| 5 | Nguyu-Kingoma(2024) | Bojomosa Agriventure Company Limited | Pwani | Mkuranga |
| 6 | Athumani H.Msumi | Saesh Business Company Limited | Pwani | Rufiji |
| 7 | Rufiji Dc | Pisah Limited | Pwani | Rufiji |
| 1 | Export Trading Company Ltd. | Zuma General Trading Company Limited | Ruvuma | Tunduru |
| 2 | Fuad Said Abdallah | Tamcu Group Of Companies Limited | Ruvuma | Tunduru |
| 3 | Ibrahimu Mohammed Ibrahimu. | Hawa Agri (T) Limited | Ruvuma | Tunduru |
| 1 | Kivukoni Muungano Agribusiness Ltd | H & E Moonrich Comapny Limited | Morogoro | ULANGA |
| 2 | Malinyi Amcos | The Prominence Global Traders And Co Ltd | Morogoro | ULANGA |
| 1 | Said Jumanne Myomba | Dreams On Development Company Limited | Singida | Manyoni |
| 1 | Mohamed Salim-Tanga Tc | Demuton Tanzania Ltd | Tanga | Tanga CC |

## 8.2 Ukusanyaji na utoaji korosho ghalani

### 8.2.1 Ukusanyaji korosho ghala kuu

Ukusanyaji wa Korosho katika Ghala Kuu chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala hadi kufikia tarehe 28 Machi 2025 ulifikia jumla ya **tani 409,164.254** kwa nchi nzima. Kimkoa zilikuwa zimekusanywa Lindi **(tani 115,680.505)**, Mtwara **(tani 240,855.731)**, Pwani **(tani 20,017.367),** Ruvuma **(tani 31,615.304),** Morogoro **(tani 390.145),** Singida **(tani 172.458 )** na Tanga **(tani 432.745)** *(Jedwali na Kielelezo Na.2.1)*




**Kielelezo Na.2.1: Ukusanyaji Korosho Ghala Kuu Msimu *2024/2025***

Katika makusanyo hayo **tani 390,329.234** sawa na **95%** ya Korosho yote chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ilikusanywa kama **Daraja la Kwanza** na **tani 18,835.021** sawa na **5%** pekee ilikusanywa kama **Daraja la Pili.**

*Ukusanyaji Korosho Ghala Kuu Msimu 2024/2025*

| Na. | Ghala | Mwendesha Ghala | Mkoa | Wilaya | Chama Kikuu | Uzito (Kg) | Daraja | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | Uliopokelewa (Kg) | Daraja I (Kg) | Daraja II (Kg) | |
| 1 | Kilwa DC. | Tanyusa Company Ltd | Lindi | Kilwa Lindi | Lindi | 6,015,577 | | | |
| 2 | Buco Lindi Cashew Nut | Sumajkt Logistic | Lindi | Lindi | Mwambao | 11,034,553 | 5,836,394 | 179,183 | |
| 3 | Industries Limited | Company Limited | Lindi | Lindi Vijijini | Lindi | 4,010,260 | 10,722,223 | | |
| 4 | Gpsa | Demuton Tanzania Ltd | Lindi | Lindi Vijijini | Mwambao | 5,639,045 | 3,751,239 | 312,330 | |
| 5 | Ilulu Cooperative Union | Kumahanda General | Lindi | Liwale | Lindi | 15,154,450 | | | |
| 6 | Limited Treasury | Supply | Lindi | Liwale | Mwambao | 10,390,924 | 5,639,045 | 259,021 | |
| 7 | Register. Hassani | Tanyusa Company Ltd | Lindi | Nachingwea | Lindi | 9,302,485 | 15,154,450 | | - |
| 8 | Yassini Mpako Umoja | Liwale Tabasamu | Lindi | Nachingwea | Mwambao | 11,707,578 | | | - |
| 9 | Amcos Ltd. | Company Limited | Lindi | Nachingwea | Lindi | 7,870,937 | 10,062,430 | | |
| 10 | Epza (Lindi Farmers Ltd) | Zuma General Trading | Lindi | Nachingwea | Mwambao | 2,449,926 | 8,631,994 | 328,494 | |
| 11 | Export Trading Company | Company Limited | Lindi | Nachingwea | RUNALI | 2,748,257 | 11,707,578 | | |
| 12 | Limited | Ahn & Raka Company | Lindi | Nachingwea | RUNALI | 5,797,553 | 7,191,523 | 670,491 | |
| 13 | Ibrahimu Somea Mushangani | Ltd | Lindi | Ruangwa | RUNALI | 759,948 | | | - |
| 14 | Lijawa | Zuma General Trading | Lindi | Ruangwa | RUNALI | 10,641,237 | 2,127,478 | | |
| 15 | Nachingwea Dc. | Company Limited | Lindi | | RUNALI | 12,157,775 | | 679,414 | |
| | Shamshu Feroz. Ibrahim | Miki General Traders | | Masasi | RUNALI | **115,680,505** | 2,570,359 | | |
| 1 | Lipande-Ruangwa Dc | Company Ltd | Mtwara | Masasi | RUNALI | | | 322,448 | |
| | | | | | | 1,906,293 | | | |
| 2 | Runali Cooperative Union | Stecuria Investment | Mtwara | Masasi | RUNALI | | 5,797,553 | | |
| | | | | | | 4,171,941 | | | |
| 3 | Limited **Jumla ndogo Lindi** | Company Limited | Mtwara | Masasi | RUNALI | | 759,948 | 177,898 | |
| | | | | | | 1,818,879 | 10,641,237 | | |
| 4 | | Lenzaq Holdings | Mtwara | Masasi | RUNALI | | | | - |
| | Afrisian Ginning Ltd- | Limited | | | | 13,599,201 | | | |
| 5 | Mtandi Ali Mohamed | | Mtwara | Masasi | | 12,258,053 | | | - |
| | | | | | | | 12,157,775 | | |
| 6 | Salim (Millenium). | The Prominence Global | Mtwara | Masasi | MAMCU | 29,235,980 | **112,751,226** | | - |
| 7 | | Traders And Co Ltd | Mtwara | Mtwara | MAMCU | | | | - |
| | Chisonga Mamcu Ltd. | | | | | 3,499,349 | | | |
| 8 | Masasi Dc | Ruangwa | Mtwara | Mtwara MC | MAMCU | 13,400,476 | | | |
| | | Warehousing | | | | | | 2,929,279 | |
| 9 | Micronix System Ltd - | Company Ltd | Mtwara | Nanyamba TC | MAMCU | 6,196,656 | 1,413,498 | | |
| 10 | Warehouse 1&2 Remigio V. | Ahn & Raka | Mtwara | Nanyumbu | MAMCU | 16,490,382 | | | |
| 11 | Naga. | Company Ltd | Mtwara | Nanyumbu | MAMCU | 2,994,169 | 4,171,941 | 492,795 | |
| 12 | Olam Limited | | Mtwara | Nanyumbu | MAMCU | 9,865,051 | | | - |
| 13 | Cashewnut Company (2005) | | Mtwara | Nanyumbu Newala | MAMCU | 4,696,655 | 1,818,879 | | - |
| 14 | Limited Mamcu Ltd Nanyamba | D&B Agribusiness | Mtwara | Newala | MAMCU | 413,934 | 12,793,783 | | |
| 15 | Libenga Investment Ltd. | Co.Ltd | Mtwara | Newala | MAMCU | 34,318,129 | | 805,418 | |
| 16 | Mamcu Ltd | Mtambaswala Company | Mtwara | Newala | MAMCU | 14,400,633 | 12,191,742 | 66,311 | |
| 17 | Mohamed Kossa Abdallah | Limited | Mtwara | Tandahimba | MAMCU | 30,222,594 | | 263,156 | |
| 18 | Yusra Hamza. Said | Perfect Cashew Kernel | Mtwara | | MAMCU | 5,100,657 | 28,972,824 | | - |
| 19 | Micronix System Limited - | Ltd | Mtwara | Kibaha | MAMCU | 36,266,699 | 3,499,349 | | |
| | Warehouse 1&2. | Mikat Agribusiness Ltd | | Kibiti | TANECU | **240,855,731** | 12,984,271 | 416,205 | |
| 1 | Tanecu Limited - Newala. | Mandiwa Agro Products | Pwani | Kibiti | TANECU | | 5,074,101 | | |
| 2 | Tanecu Limited | Limited | Pwani | Mafia | TANECU | 1,547,794 | 15,511,848 | 1,122,555 | |
| 3 | (Agrofocus) Tanecu | Makita Agrifood Limited | Pwani | Mkuranga | TANECU | 5,999,769 | 2,892,714 | | |
| 4 | Ltd-Chiwonga Tanecu | Vika General Company | Pwani | Rufiji | TANECU | 3,165,919 | | 978,534 | |
| 5 | Ltd - Tandahimba. | Limited | Pwani | Rufiji | | 54,248 | 9,777,548 | | |
| 6 | **Jumla ndogo Mtwara** | Nampachila Business | Pwani | | CORECU | 2,912,746 | | 101,455 | |
| 7 | | Company Limited | Pwani | Tunduru | CORECU | 1,698,014 | 4,696,655 | 87,503 | |
| | Misugusugu Amcos Limited | Mufena Company | | Tunduru | CORECU | 4,638,877 | 413,934 | | - |
| | Corecu (1984) Ltd - A & B | Limited | | | CORECU | **20,017,367** | 33,376,759 | | - |
| 1 | Juma Ally Ngwaya - Bungu | Mkaba General Traders | Ruvuma | Tunduru | CORECU | | | | |
| 2 | Kiegeani | Co.Limited | Ruvuma | | CORECU | 12,642,800 | 13,982,673 | | |
| 3 | Nguyu-Kingoma(2024) | Bojomosa Agriventure | Ruvuma | ULANGA | CORECU | 11,925,519 | | 941,370 | |
| | Athumani H.Msumi | Company Limited | | ULANGA | CORECU | 7,046,985 | 28,843,499 | | |
| 1 | Rufiji Dc | Geju Investment And | Morogor | | | **31,615,304** | 4,513,474 | 417,960 | |
| 2 | **Jumla ndogo Pwani** | General Supply | o | Manyoni | TAMCU | 181,468 | 35,084,138 | | |
| | Export Trading Company Ltd. | Company Limited | Morogor | | TAMCU | 208,677 | **232,013,630** | 1,379,095 | |
| 1 | Fuad Said Abdallah | Twenyuka Company | o | Tanga CC | TAMCU | **390,145** | | 587,183 | |
| | Ibrahimu Mohammed | Limited | | | | | | | |
| 1 | Ibrahimu. Jumla ndogo | Dreams On | Singida | | MOFACU | 172,458 | 749,918 | 1,182,561 | |
| | Ruvuma | Development Company | | | MOFACU | **172,458** | 3,714,151 | **8,842,101** | |
| | | Limited | Tanga | | | 432,745 | | | |
| | Kivukoni Muungano | Cropstan Investment | | | SIFACU | **432,745** | 2,186,053 | | |
| | Agribusiness Ltd | Limited | | | | | 34,720 | 797,876 | |
| | Malinyi Amcos | Ace Global Depository | | | TACACU | | 1,365,520 | | |
| | **Jumla ndogo Morogoro** | (T) Limited | | | | | | 2,285,618 | |
| | | Sb Logistics & | | | | | 1,698,014 | | |
| | Said Jumanne | Company Limited | | | | | | 979,866 | |
| | Myomba **Jumla** | Dreams On | | | | | 3,904,504 | 19,528 | |
| | **ndogo Singida** | Development Company | | | | | **13,652,880** | 1,547,226 | |
| | | Limited | | | | | | | - |
| | Mohamed Salim-Tanga Tc | Bin Swalehe General | | | | | | | |
| | **Jumla ndogo Tanga** | Dealers Ltd | | | | | 12,534,007 | 734,373 | |
| | | | | | | | 11,908,365 | **6,364,487** | |
| | | Zuboma General | | | | | 7,014,076 | | |
| | | Supplies | | | | | **31,456,448** | 108,793 | |
| | | Krenk Agro (T) Ltd | | | | | | 17,154 | |
| | | Pugna Agrofood | | | | | 169,223 | | |
| | | Tanzania Ltd | | | | | | 32,909 | |
| | | Mafia Cashewnut & | | | | | | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Coconut Cooperative Society | | 147,981<br>**317,204** | **158,856** |
| | Bojomosa Agriventure Company Limited | | | |
| | Saesh Business Company Limited | | 128,700<br>**128,700** | 12,245 |
| | Pisah Limited | | 9,146 | 60,696<br>**72,941** |
| | Zuma General Trading Company Limited | | **9,146** | 43,758<br>**43,758** |
| | Tamcu Group Of Companies Limited | | | |
| | Hawa Agri (T) Limited | | | 423,599<br>**423,599** |
| | H & E Moonrich Comapny Limited | | | |
| | The Prominence Global Traders And Co Ltd | | | |
| | Dreams On Development Company Limited | | | |
| | Demuton Tanzania Ltd | | | |
| 48 | **Grand Total** | **409,164,254** | **390,329,234** | **18,835,021** |

## 8.2.2 Utoaji Korosho Ghala Kuu

Utoaji wa Korosho katika Ghala Kuu chini ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala hadi kufikia tarehe 28 Machi 2025 katika **tani 409,164.254** zilizopokelewa nchi nzima; palitokea upungufu wa tani **1,533.014** sawa na **0.37%** hivyo kufanya kiasi halisi kilichotoka kuwa sawa na **tani 407,631.240** ***(Jedwali Na.2.2)***. Kwa mujibu wa taratibu za kimwongozo, kila upungufu uliobainika na kuripotiwa kupitia Fomu Namba 7 uliwasilishwa kwa Bodi ya Korosho kwa ajili ya malipo. Malipo hayo yatafanyika kwa kutumia fedha ya Tsh 7 iliyokusanywa na kuhifadhiwa katika mfuko wa zao, kwa madhumuni ya kufidia matukio yanayosababisha kushuka kwa thamani ya korosho iliyokusanywa ghalani.


**Utoaji Korosho Ghala Kuu Msimu 2024/2025**

| N | Ghala | Mwendesha Ghala | Mkoa | Wilaya | Chama Kikuu | Uliopokelewa (Kg) | Taarifa za Fomu Namba 7 Upungufu (Kg) | Tofauti (Kg) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kilwa DC. | Tanyusa Company Ltd | Lindi | Kilwa | Lindi | | | 0.39% |
| 2 | Buco Lindi Cashew Nut | Sumajkt Logistic Company Limited | Lindi | Lindi | Mwambao | 6,015.577 | 23.260 | 0.01% |
| 3 | Industries Limited | Demuton Tanzania Ltd | Lindi | Lindi | Lindi | | 0.740 | 0.25% |
| 4 | Gpsa | Kumahanda General Supply | Lindi | Lindi Vijijini | Mwambao | 11,034.553 | 10.063 | 0.45% |
| 5 | Ilulu | Tanyusa Company Ltd | Lindi | Lindi Vijijini | Lindi | | 25.430 | 0.81% |
| 6 | Cooperative | Liwale Tabasamu Company Limited | Lindi | Liwale | Mwambao | 4,010.260 | 122.148 | 0.08% |
| 7 | Union Limited | Zuma General Trading Company | Lindi | Liwale | Lindi | | 8.566 | 0.64% |
| 8 | Treasury | Limited | Lindi | Nachingwea | Mwambao | 5,639.045 | | 0.41% |
| 9 | Register. | Ahn & Raka Company Ltd | Lindi | Nachingwea | Lindi | | 59.537 | 0.48% |
| 10 | Hassani | Zuma General Trading Company | Lindi | Nachingwea | Mwambao | 15,154.450 | 48.519 | 1.41% |
| 11 | Yassini Mpako | Limited | Lindi | Nachingwea | RUNALI | | 37.702 | 0.33% |
| 12 | Umoja Amcos | Miki General Traders Company Ltd | Lindi | Nachingwea | RUNALI | 10,390.924 | 34.569 | 0.43% |
| 13 | Ltd. | Stecuria Investment Company Limited | Lindi | Nachingwea | RUNALI | | | 0.00% |
| 14 | Epza (Lindi Farmers Ltd) | Lenzaq Holdings Limited | Lindi | Ruangwa | RUNALI | 9,302.485 | 8.984 | 0.55% |
| 15 | Export Trading Company | The Prominence Global Traders And | Lindi | Ruangwa | RUNALI | | | 0.45% |
| | Limited | Co Ltd | | | RUNALI | 11,707.578 | 24.793 | **0.45%** |
| 1 | Ibrahimu Somea Mushangani | Ruangwa Warehousing Company Ltd | Mtwara | Masasi | RUNALI | | | 0.32% |
| 2 | Lijawa | Ahn & Raka Company Ltd | Mtwara | Masasi | RUNALI | 7,870.937 | - | 0.84% |
| 3 | Nachingwea Dc. | | Mtwara | Masasi | RUNALI | | | 0.65% |
| 4 | Shamshu Feroz. Ibrahim | D&B Agribusiness Co.Ltd | Mtwara | Masasi | RUNALI | 2,449.926 | 58.237 | 0.37% |
| 5 | Lipande-Ruangwa Dc | Mtambaswala Company Limited | Mtwara | Masasi | | | 54.891 | 0.42% |
| 6 | Runali | Perfect Cashew Kernel Ltd | Mtwara | Masasi | MAMCU | 2,748.257 | **517.439** | 0.28% |
| 7 | Cooperative | Mikat Agribusiness Ltd | Mtwara | Masasi | MAMCU | | | 1.58% |
| 8 | Union Limited | Mandiwa Agro Products Limited | Mtwara | Mtwara | MAMCU | 5,797.553 | 6.026 | 0.15% |
| 9 | **Jumla ndogo** | Makita Agrifood Limited | Mtwara | Mtwara MC | MAMCU | | | 0.63% |
| 10 | **Lindi** | Vika General Company Limited | Mtwara | Nanyamba TC | MAMCU | 759.948 | 35.156 | 0.36% |
| 11 | Afrisian | Nampachila Business Company | Mtwara | Nanyumbu | MAMCU | 10,641.237 | 11.810 | 0.36% |
| 12 | Ginning Ltd- | Limited | Mtwara | Nanyumbu | MAMCU | | 50.664 | 0.00% |
| 13 | Mtandi Ali | Mufena Company Limited | Mtwara | Nanyumbu | MAMCU | 12,157.775 | 51.451 | 0.28% |
| 14 | Mohamed | Mkaba General Traders Co.Limited | Mtwara | Nanyumbu | MAMCU | | 81.824 | 0.00% |
| 15 | Salim | Bojomosa Agriventure Company | Mtwara | Newala | MAMCU | **115,680.505** | 55.256 | 0.48% |
| 16 | (Millenium). | Limited | Mtwara | Newala | MAMCU | | 19.972 | 0.16% |
| 17 | Chisonga | Geju Investment And General Supply | Mtwara | Newala | MAMCU | 1,906.293 | 38.834 | 0.30% |
| 18 | Mamcu Ltd. | Company Limited | Mtwara | Newala | MAMCU | | 59.958 | 0.47% |
| 19 | Masasi Dc | Twenyuka Company Limited | Mtwara | Tandahimba | MAMCU | 4,171.941 | | 0.28% |
| | Micronix System Ltd | Dreams On Development Company | | | TANECU | | 10.630 | **0.35%** |
| 1 | - Warehouse 1&2 | Limited | Pwani | Kibaha | TANECU | 1,818.879 | | 0.00% |
| 2 | Remigio V. Naga. | Cropstan Investment Limited | Pwani | Kibiti | TANECU | | - | 0.29% |
| 3 | Olam Limited | Ace Global Depository (T) Limited | Pwani | Kibiti | TANECU | 13,599.201 | | 0.17% |
| 4 | Cashewnut | Sb Logistics & Company Limited | Pwani | Mafia | TANECU | | 12.950 | 0.00% |
| 5 | Company (2005) | Dreams On Development Company | Pwani | Mkuranga | | 12,258.053 | | 0.23% |
| 6 | Limited Mamcu Ltd | Limited | Pwani | Rufiji | CORECU | | - | 0.00% |
| 7 | Nanyamba | Bin Swalehe General Dealers Ltd | Pwani | Rufiji | CORECU | 29,235.980 | | 0.14% |
| | Libenga | | | | CORECU | | 163.680 | **0.18%** |
| 1 | Investment | Zuboma General Supplies | Ruvuma | Tunduru | CORECU | 3,499.349 | | |
| 2 | Ltd. Mamcu | Krenk Agro (T) Ltd | Ruvuma | Tunduru | CORECU | | 23.229 | 0.55% |
| 3 | Ltd | Pugna Agrifood Tanzania Ltd | Ruvuma | Tunduru | CORECU | 13,400.476 | 91.259 | 0.40% |
| | Mohamed Kossa Abdallah | Mafia Cashewnut & Coconut | | | CORECU | | 24.002 | 0.33% |
| 1 | Yusra Hamza. Said | Cooperative Society | Morogoro | ULANGA | | 6,196.656 | | **0.45%** |
| 2 | Micronix System Limited - | Bojomosa Agriventure Company | Morogoro | ULANGA | TAMCU | | 101.226 | 0.00% |
| | Warehouse 1&2. | Limited | | | TAMCU | 16,490.382 | | 0.00% |
| 1 | Tanecu Limited - Newala. | Saesh Business Company Limited | Singida | Manyoni | TAMCU | | **837.927** | - |
| | Tanecu | Pisah Limited | Tanga | | | 2,994.169 | | |
| 1 | Limited | | | Tanga CC | MOFACU | | | 0.00% |
| | (Agrofocus) | Zuma General Trading Company | | | MOFACU | 9,865.051 | - | - |
| | Tanecu Ltd- | Limited | | | | | | |
| | Chiwonga | Tamcu Group Of Companies | | | SIFACU | 4,696.655 | 17.698 | 0.00% |
| | Tanecu Ltd - | Limited Hawa Agri (T) Limited | | | | | | - |
| | Tandahimba. | | | | TACACU | 413.934 | 5.509 | |
| | **Jumla** | H & E Moonrich Comapny Limited | | | | 34,318.129 | - | |
| | **ndogo** | The Prominence Global Traders | | | | | | |
| | **Mtwara** | | | | | 14,400.633 | 6.564 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Misugusugu | And Co Ltd Dreams On | | | |
| | Amcos Limited | | 30,222.594 | - | |
| | Corecu (1984) | | | | |
| | Ltd - A & B | Development Company Limited | 5,100.657 | 6.371 | |
| | Juma Ally Ngwaya - Bungu | | | | |
| | Kiegeani | | 36,266.699 | **36.142** | |
| | Nguyu-Kingoma(2024) | Demuton Tanzania Ltd | | | |
| | Athumani H.Msumi | | **240,855.731** | 70.095 | |
| | Rufiji Dc | | | 48.193 | |
| | **Jumla ndogo Pwani** | | 1,547.794 | 23.218 | |
| | Export Trading Company Ltd. | | | | |
| | Fuad Said Abdallah | | 5,999.769 | **141.506** | |
| | Ibrahimu | | | | |
| | Mohammed | | 3,165.919 | - | |
| | Ibrahimu. Jumla | | | | |
| | ndogo Ruvuma | | 54.248 | - | |
| | | | 2,912.746 | | |
| | Kivukoni Muungano | | | | |
| | Agribusiness Ltd | | 1,698.014 | - | |
| | Malinyi Amcos | | | | |
| | **Jumla ndogo Morogoro** | | 4,638.877 | - | |
| | Said | | | | |
| | Jumanne | | **20,017.367** | - | |
| | Myomba | | | | |
| | **Jumla** | | 12,642.800 | - | |
| | **ndogo** | | | | |
| | **Singida** | | 11,925.519 | - | |
| | Mohamed Salim-Tanga Tc | | | | |
| | **Jumla ndogo Tanga** | | 7,046.985 | | |
| | | | **31,615.304** | | |
| | | | 181.468 | | |
| | | | 208.677 | | |
| | | | **390.145** | | |
| | | | 172.458 | | |
| | | | **172.458** | | |
| | | | 432.745 | | |
| | | | **432.745** | | |
| 48 | **Jumla Kuu** | | **409,164.254** | **1,533.014** | **0.37%** |

### 8. 2.3. Bei na mapato

Katika msimu wa 2024/2025 Korosho iliyokusanywa na kuuzwa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala *(hii haihusu korosho iliyouzwa nje ya mfumo)* wastani wa bei ulikuwa **Sh. 3,104.24.** Thamani ya Korosho iliyouzwa ilikuwa **Sh. Trilioni 1.28**. Mkoa ulioongoza kwa mapato ni mkoa wa Mtwara ulikuwa na Korosho yenye thamani ya **Sh. Bilioni 763.4**; ikifuatiwa na **Lindi Sh. Bilioni 363.2; Ruvuma Sh. Billioni 93.1**; **Pwani Sh. Bilioni 58.7**; **Singida Milioni 499.9**, **Tanga Sh. Bilioni 1.1** na **Morogoro Sh. Bilioni 1.0** *(Jedwali 2.3 na Kielelezo Na.2.3)*.




***Kielelezo Na.2.3: Mapato Kimkoa Msimu wa Korosho 2024/2025***

**Jedwali Na.10: Mapato na Bei Kimkoa Msimu wa Korosho 2024/2025**

| Na. | Ghala | Mwendesha ghala | Mkoa | Wilaya | Chama kikuu | Bei (Tsh) | Thamani (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kilwa DC. | Tanyusa Company Ltd | Lindi | Kilwa | Lindi Mwambao | 3,063.24 | 18,564,001,503.33 |
| 2 | Buco Lindi Cashew Nut Industries Limited | Sumajkt Logistic Company Limited | Lindi | Lindi | Lindi Mwambao | 3,172.71 | 34,744,108,668.85 |
| 3 | Gpsa | Demuton Tanzania Ltd | Lindi | Lindi | Lindi Mwambao | 3,101.35 | 12,393,204,986.00 |
| 4 | Ilulu Cooperative Union Limited | Kumahanda General Supply | Lindi | Lindi Vijijini | Lindi Mwambao | 2,968.00 | 16,862,269,321.67 |
| 5 | Treasury Register. | Tanyusa Company Ltd | Lindi | Lindi Vijijini | Lindi Mwambao | 3,158.62 | 48,005,998,510.58 |
| 6 | Hassani Yassini Mpako | Liwale Tabasamu Company Limited | Lindi | Liwale | RUNALI | 3,045.65 | 31,984,057,504.63 |
| 7 | Umoja Amcos Ltd. | Zuma General Trading Company Limited | Lindi | Liwale | RUNALI | 3,003.16 | 28,338,891,770.00 |
| 8 | Epza (Lindi Farmers Ltd) | Ahn & Raka Company Ltd | Lindi | Nachingwea | RUNALI | 3,318.94 | 38,915,902,698.57 |
| 9 | Export Trading Company Limited | Zuma General Trading Company Limited | Lindi | Nachingwea | RUNALI | 2,923.65 | 23,026,967,850.00 |
| 10 | Ibrahimu Somea Mushangani | Miki General Traders Company Ltd | Lindi | Nachingwea | RUNALI | 2,481.83 | 6,008,601,164.93 |
| 11 | Lijawa | Stecuria Investment Company Limited | Lindi | Nachingwea | RUNALI | 2,956.12 | 8,114,159,520.00 |
| 12 | Nachingwea Dc. | Lenzaq Holdings Limited | Lindi | Nachingwea | RUNALI | 3,133.16 | 18,287,149,240.00 |
| 13 | Shamshu Feroz. Ibrahim | The Prominence Global Traders And Co Ltd | Lindi | Nachingwea | RUNALI | 3,069.64 | 2,363,414,100.00 |
| 14 | Lipande-Ruangwa Dc | Ruangwa Warehousing Company Ltd | Lindi | Ruangwa | RUNALI | 3,321.21 | 35,540,082,878.33 |
| 15 | Runali Cooperative Union Limited | Ahn & Raka Company Ltd | Lindi | Ruangwa | RUNALI | 3,289.10 | 40,089,991,107.00 |
| | **Jumla ndogo Lindi** | | | | | **3,067.09** | **363,238,800,823.89** |
| 1 | Afrisian Ginning Ltd-Mtandi | D&B Agribusiness Co.Ltd | Mtwara | Masasi | MAMCU | 2,508.22 | 4,785,769,080.00 |
| 2 | Ali Mohamed Salim (Millenium). | Mtambaswala Company Limited | Mtwara | Masasi | MAMCU | 2,963.58 | 12,500,462,369.00 |
| 3 | Chisonga | Perfect Cashew Kernel Ltd | Mtwara | Masasi | MAMCU | 2,799.01 | 5,131,948,080.00 |
| 4 | Mamcu Ltd. | Mikat Agribusiness Ltd | Mtwara | Masasi | MAMCU | 2,907.57 | 39,166,822,405.00 |
| 5 | Masasi Dc | Mandiwa Agro Products Limited | Mtwara | Masasi | MAMCU | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | 3,429.38 | 42,159,075,072.40 |
| 6 | Micronix System Ltd - Warehouse 1&2 | Makita Agrifood Limited | Mtwara | Masasi | MAMCU | 3,386.56 | 98,655,294,917.67 |
| 7 | Remigio V. Naga. | Vika General Company Limited | Mtwara | Masasi | MAMCU | 2,812.01 | 9,883,490,470.00 |
| 8 | Olam Limited | Nampachila Business Company Limited | Mtwara | Mtwara | MAMCU | 2,968.31 | 39,800,944,123.67 |
| 9 | Cashewnut Company (2005) Limited | Mufena Company Limited | Mtwara | Mtwara MC | MAMCU | 2,541.82 | 15,874,475,004.85 |
| 10 | Mamcu Ltd Nanyamba | Mkaba General Traders Co.Limited | Mtwara | Nanyamba TC | MAMCU | 3,019.15 | 50,141,620,243.33 |
| 11 | Libenga Investment Ltd. | Bojomosa Agriventure Company Limited | Mtwara | Nanyumbu | MAMCU | 3,252.00 | 9,918,989,780.00 |
| 12 | Mamcu Ltd | Geju Investment And General Supply Company Limited | Mtwara | Nanyumbu | MAMCU | 3,354.69 | 32,959,159,386.32 |
| 13 | Mohamed Kossa Abdallah | Twenyuka Company Limited | Mtwara | Nanyumbu | MAMCU | 3,077.36 | 14,556,962,527.62 |
| 14 | Yusra Hamza. Said | Dreams On Development Company Limited | Mtwara | Nanyumbu | MAMCU | 3,208.65 | 1,331,174,940.00 |
| 15 | Micronix System Limited - Warehouse 1&2. | Cropstan Investment Limited | Mtwara | Newala | TANECU | 3,263.97 | 112,526,763,083.61 |
| 16 | Tanecu Limited - Newala. | Ace Global Depository (T) Limited | Mtwara | Newala | TANECU | 3,099.18 | 44,939,897,645.00 |
| 17 | Tanecu Limited (Agrofocus) | Sb Logistics & Company Limited | Mtwara | Newala | TANECU | 3,233.63 | 97,637,383,535.00 |
| 18 | Tanecu Ltd-Chiwonga | Dreams On Development Company Limited | Mtwara | Newala | TANECU | 2,735.99 | 13,985,720,730.50 |
| 19 | Tanecu Ltd - Tandahimba. | Bin Swalehe General Dealers Ltd | Mtwara | Tandahimba | TANECU | 3,233.55 | 117,466,402,524.33 |
| | **Jumla ndogo Mtwara** | | | | | **3,041.82** | **763,422,355,918.29** |
| 1 | Misugusugu Amcos Limited | Zuboma General Supplies | Pwani | Kibaha | CORECU | 2,790.66 | 4,378,496,671.13 |
| 2 | Corecu (1984) Ltd - A & B | Krenk Agro (T) Ltd | Pwani | Kibiti | CORECU | 2,833.23 | 17,149,696,570.36 |
| 3 | Juma Ally Ngwaya - Bungu | Pugna Agrifood Tanzania Ltd | Pwani | Kibiti | CORECU | 2,972.58 | 9,423,637,460.00 |
| 4 | Kiegeani | Mafia Cashewnut & Coconut Cooperative Society | Pwani | Mafia | CORECU | 2,810.00 | 152,436,880.00 |
| 5 | Nguyu-Kingoma(2024) | Bojomosa Agriventure Company Limited | Pwani | Mkuranga | CORECU | 2,640.08 | 7,774,672,855.00 |
| 6 | Athumani H.Msumi | Saesh Business Company Limited | Pwani | Rufiji | CORECU | 3,350.64 | 5,702,552,280.00 |
| 7 | Rufiji Dc | Pisah Limited | Pwani | Rufiji | CORECU | 2,995.19 | 14,103,417,020.00 |
| | **Jumla ndogo Pwani** | | | | | **2,913.20** | **58,684,909,736.48** |
| 1 | Export Trading Company Ltd. | Zuma General Trading Company Limited | Ruvuma | Tunduru | TAMCU | 2,903.98 | 36,847,153,931.44 |
| 2 | Fuad Said Abdallah | Tamcu Group Of Companies Limited | Ruvuma | Tunduru | TAMCU | 2,956.38 | 35,452,304,938.33 |
| 3 | Ibrahimu Mohammed Ibrahimu. | Hawa Agri (T) Limited | Ruvuma | Tunduru | TAMCU | 2,940.89 | 20,753,913,719.67 |
| | Jumla ndogo Ruvuma | | | | | **2,933.75** | **93,053,372,589.44** |
| 1 | Kivukoni Muungano Agribusiness Ltd | H & E Moonrich Comapny Limited | Morogoro | ULANGA | MOFACU | 2,501.18 | 472,475,380.00 |
| 2 | Malinyi Amcos | The Prominence Global Traders And Co Ltd | Morogoro | ULANGA | MOFACU | 2,631.95 | 554,394,020.00 |
| | **Jumla ndogo Morogoro** | | | | | **2,501.18** | **1,026,869,400.00** |
| 1 | Said Jumanne Myomba | Dreams On Development Company Limited | Singida | Manyoni | SIFACU | 2,744.20 | 499,922,280.00 |
| | **Jumla ndogo Singida** | | | | | **2,744.20** | **499,922,280.00** |
| 1 | Mohamed Salim-Tanga Tc | Demuton Tanzania Ltd | Tanga | Tanga CC | TACACU | 2,467.36 | 1,090,074,791.87 |
| | **Jumla ndogo Tanga** | | | | | **2,467.36** | **1,090,074,791.87** |
| 48 | **Jumla Kuu** | | | | | **3,104.24** | **1,281,016,305,539.98** |

### 8.3 Hali ya utendaji wa wadau mbalimbali

Sehemu hii inajadili utendaji wa wadau wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ikiwemo wakulima, wanunuzi na Waendesha Ghala kwa kutazama takwimu muhimu jinsi walivyofanya katika msimu wa Korosho 2024/2025.

#### 8.3.1. Waweka mali (Wakulima) Vyama vya Msingi (AMCOS)

Katika Msimu wa 2024/2025 jumla ya **Waweka Mali** (**AMCOS) 1132** zilikusanya Korosho katika Ghala Kuu mbalimbali. Takwimu muhimu za AMCOS hizo ni kama ifuatavyo:

##### 8.3.1.1. AMCOS zilizoongoza kwa makusanyo

Kwa mujibu wa takwimu katika Kanzidata ya WRRB, **AMCOS ya Tuaminiane Rural Primary Cooperative Society** kutokea mkoa wa Mtwara wilayani Masasi ndiyo iliyoongoza kwa kukusanya **tani 2,218.589**; orodha ya AMCOS Kumi Bora katika makusanyo ni kama inavyoonekana katika *Jedwali Na.11*.

**Jedwali Na.11: AMCOS Kumi Bora kwa Makusanyo Msimu 2024/2025**

| N | Mkoa | Wilaya | AMCOS | Uzito Uliopokelewa (Kg) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mtwara | Masasi | Tuaminiane Rural Primary Cooperative Society | 2,218,589 |
| 2 | Mtwara | Newala | Kitangari Amcos Ltd | 2,134,819 |
| 3 | Lindi | Lindi Vijijini | Nyengedi Amcos Ltd | 2,112,070 |
| 4 | Lindi | Liwale | Umoja Amcos Ltd | 2,011,832 |
| 5 | Lindi | Lindi Vijijini | Mtama Amcos Ltd | 1,629,914 |
| 6 | Lindi | Ruangwa | Luchelegwa Amcos Ltd | 1,618,730 |
| 7 | Lindi | Ruangwa | Mandawa Amcos Ltd | 1,609,165 |
| 8 | Lindi | Lindi Vijijini | Kiwalala Amcos Ltd | 1,605,423 |
| 9 | Lindi | Lindi Vijijini | Nyangao Amcos Ltd | 1,583,618 |
| 10 | Ruvuma | Tunduru | Namitili Amcos Ltd | 1,580,794 |

### 3.1.2. AMOCS zilizoongoza kwa kukusanya Daraja la Kwanza

Kwa mujibu wa takwimu katika Kanzidata ya WRRB, **AMCOS ya Tuaminiane Rural Primary Cooperative Society** kutokea mkoa wa Mtwara wilayani Masasi, ndiyo iliyoongoza kwa kukusanya **tani 2,159.049** zilizokuwa na wastani wa **SOT ya 51**, **unyevu (MC) 9.1%** na **Idadi ya Punje (NC) 166**. Orodha ya AMCOS Kumi Bora kwa waliokusanya Daraja la I kama inavyoonekana katika *Jedwali Na.12*.

**Jedwali Na.12: AMCOS Kumi Bora kwa Daraja la I Msimu 2024/2025**

| N | Mkoa | Wilaya | AMCOS | Daraja I (Kg) | SOT | Moisture (%w/w) | Nut Count |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mtwara | Masasi | Tuaminiane Rural Primary Cooperative Society | 2,159,049 | 51 | 9.1 | 166 |
| 2 | Mtwara | Newala | Kitangari Amcos Ltd | 2,124,954 | 52 | 9.2 | 167 |
| 3 | Lindi | Lindi Vijijini | Nyengedi Amcos Ltd | 2,112,070 | 50 | 9.0 | 173 |
| 4 | Lindi | Liwale | Umoja Amcos Ltd | 1,882,461 | 50 | 8.5 | 165 |
| 5 | Lindi | Lindi Vijijini | Mtama Amcos Ltd | 1,629,914 | 51 | 9.0 | 174 |
| 6 | Lindi | Ruangwa | Luchelegwa Amcos Ltd | 1,618,730 | 52 | 8.5 | 167 |
| 7 | Lindi | Ruangwa | Mandawa Amcos Ltd | 1,609,165 | 52 | 8.5 | 186 |
| 8 | Lindi | Lindi Vijijini | Kiwalala Amcos Ltd | 1,605,423 | 50 | 9.0 | 175 |
| 9 | Lindi | Lindi Vijijini | Nyangao Amcos Ltd | 1,583,618 | 51 | 8.9 | 170 |
| 10 | Ruvuma | Tunduru | Namitili Amcos Ltd | 1,580,794 | 51 | 8.3 | 184 |

### 8.3.1.3. AMOCS zilizoongoza kwa mapato ya korosho

Kwa mujibu wa takwimu katika Kanzidata ya WRRB, **AMCOS ya Liwale** kutokea mkoa wa Lindi wilayani Liwale pia, ndiyo iliyoongoza kwa kupata wastani wa thamani ya **Sh. Bilioni 7.02** katika mauzo ya Korosho Msimu 2024/2025. Orodha ya AMCOS Kumi Bora kwa mapato ni kama inavyoonekana katika *Jedwali Na.13*.

**Jedwali Na.13: AMCOS Kumi Bora kwa Mapato Msimu 2024/2025**

| N | Mkoa | Wilaya | AMCOS | Wastani Bei (Tsh) | Mapato (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mtwara | Masasi | Tuaminiane Rural Primary Cooperative Society | 3,081.45 | 7.02 Bilioni |
| 2 | Mtwara | Newala | Kitangari Amcos Ltd | 3,255.51 | 6.99 Bilioni |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Lindi | Lindi Vijijini | Nyengedi Amcos Ltd | 3,082.32 | 6.55 Bilioni |
| 4 | Lindi | Liwale | Umoja Amcos Ltd | 2,950.92 | 6.17 Bilioni |
| 5 | Lindi | Ruangwa | Mandawa Amcos Ltd | 3,321.41 | 5.38 Bilioni |
| 6 | Lindi | Ruangwa | Luchelegwa Amcos Ltd | 3,207.00 | 5.26 Bilioni |
| 7 | Mtwara | Masasi | Nangoo Rural Primary Cooperative Society | 3,313.38 | 5.24 Bilioni |
| 8 | Lindi | Lindi Vijijini | Mtama Amcos Ltd | 3,118.67 | 5.10 Bilioni |
| 9 | Lindi | Lindi Vijijini | Kiwalala Amcos Ltd | 3,123.94 | 5.04 Bilioni |
| 10 | Lindi | Lindi Vijijini | Nyangao Amcos Ltd | 3,096.36 | 4.95 Bilioni |

### 8.3.2. Wanunuzi

Katika Msimu wa 2024/2025 jumla ya **Kampuni 83** za **Wanunuzi,** walijitokeza kununua na kushinda minada iliyokuwa ikifanyika kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala *(Kiambatisho Na. 2)*. Takwimu muhimu za Wanunuzi hizo ni kama ifuatavyo.

#### 3.2.1. Wanunuzi walioongoza kununua kiasi cha korosho

Kwa mujibu wa takwimu katika Kanzidata ya WRRB, **Export Trading Co Ltd** ndiyo iliyoongoza kwa kununua kiwango cha juu cha korosho kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Aidha, kampuni **Kumi Bora** zilinunua jumla ya **tani 229,363.779** sawa na **56%** ya Korosho yote iliyokusanywa kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Orodha ya Kampuni Kumi Bora kwa kiasi kilichonunuliwa ni kama inavyoonekana katika *Jedwali Na.14*.

**Jedwali Na.14: Kampuni Kumi Bora kwa kiasi cha manunuzi**

| N | Jina la Mnunuzi |
|---|---|
| 1 | Export Trading Company Limited |
| 2 | Iscon Commodities (T) Ltd |
| 3 | Vnbp Trading Co.Ltd |
| 4 | Alpha Namata Company Ltd |
| 5 | Kopac Company Limited |
| 6 | Dormans Tanzania Ltd |
| 7 | Dunamis Agric Ltd |
| 8 | Three Leaves Commodity (Tz) Ltd |
| 9 | Sg Trade Tanzania Limited |
| 10 | H S Impex Ltd |

#### 8.3.2.2. Wanunuzi walioongoza kwa wastani wa juu wa bei

Kwa mujibu wa takwimu katika Kanzidata ya WRRB, **Sr Impex Tanzania Ltd** ndiyo iliyoongoza kwa wastani wa bei ya juu kwa kutoa **Sh. 3,751.41.00 kwa kilo**. Aidha, kampuni tatu bora kwa wastani wa bei zilitoa wastani wa **Sh. 3,662.70**. Orodha ya Kampuni Tatu Bora kwa wastani wa bei ni kama inavyoonekana katika *Jedwali Na.15*

**Jedwali Na.15: Kampuni Kumi Bora kwa wastani wa bei**

| N | Jina la Mnunuzi | Bei Wastani (Tsh) |
|---|---|---|
| 1 | Sr Impex Tanzania Ltd | 3751.41 |
| 2 | Simba Korosho Limited | 3680.84 |
| 3 | Kasuga General Traders Limited | 3555.85 |

#### 8.3.2.3. Ufanisi wa wanunuzi kutoa mizigo ghalani kwa haraka

Kwa mujibu wa takwimu katika Kanzidata ya WRRB, wastani wa mzigo kukaa ghalani tokea siku unapopokelewa mpaka mnunuzi kuuchukua ni **siku 16**. Katika msimu wa 2024/2025 kampuni ya **T.C. Agriculture Co Ltd** ndiyo iliongoza kwa kuchukua mzigo ndani ya **siku 8** tokea kupokelewa kwake.

Muda wa mzigo kukaa ghalani hutegemea wakulima walipoanza kukusanya na kasi ya kukamilika kwa *stake* ambazo zinapofikia idadi inayotosha hupelekwa minadani; hii huweza kuchukua wastani wa siku nne hadi saba au zaidi kutegemea na eneo. Hii hufuatiwa na muda mnunuzi anaopewa kukamilisha malipo wa siku zisizopungua nne na hatimaye kuanza kutolewa pindi mnunuzi anapofika ghalani ambapo hupewa siku 14 za kazi kutoa bila adhabu.

Orodha ya Kampuni Tatu Bora kwa wastani wa siku za kutoa mzigo ghalani ni kama inavyoonekana katika *Jedwali Na.3.2.3*.

**Jedwali Na.16: Kampuni Tatu Bora kwa ufanisi wa kutoa mzigo**

| N | Jina la Mnunuzi | Siku za Kutoa Mzigo |
|---|---|---|
| 1 | T.C Agriculture Co. Ltd | 8 |
| 2 | Exodus Agro Export Ltd | 8 |
| 3 | Acorp Export Company Limited | 9 |

#### 8.3.3. Waendesha Ghala

Katika msimu wa 2024/2025 WRRB ilitoa leseni kwa jumla ya **kampuni 39** za Waendesha Ghala. Kama ilivyoatajwa katika kikao cha wadau cha tarehe 20 Julai 2021, ilipangwa kila msimu wa zao utakapokamilikaWaendesha Ghala watadarajishwa kutokana na utendaji wao. Katika udarajishaji jumla ya vigezo vikuu **vinne (4)** ambavyo ndani yake vilikuwa vimejengwa na vigezo vingine vidogo vidogo. Vigezo vilivyotumika ni kama ifuatavyo:

a. **Uzoefu:** Kipimo hiki kilikuwa na vigezo viwili ikiwemo ***kiasi cha uzito*** aliowahi kuhudumia kihistoria, ***Idadi ya Leseni ya Mazao kwa Misimu***. Kipimo hiki chote kilitumia takwimu halisi kutoka kwenye Kanzidata ya WRRB.
b. **Hatari ya Kutengeneza Madeni**: Kipimo hiki kilikuwa na vigezo viwili ikiwemo takwimu za **kiwango cha upungufu kinachooneka kwenye kanziadata** kwa kulinganisha mzigo uliongia na kutoka na kiwango cha upungufu kilichowasilishwa kupitia Fomu Namba 7 kwa kuzingatia Mwongozo.
c. **Malalamiko Kutoka kwa Wadau**: Kipimo hiki kilikuwa na vigezo viwili ikiwemo idadi ya malalamiko yaliyowasilishwa na kuthibitishwa kuwa na mashiko kutoka kwa **Wakulima** na **Wanunuzi**.
d. **Uwezo wa Kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo**: Kipimo hiki kilikuwa na vigezo viwili ambavyo vilitazama mwenendo wa Mwendesha Ghala na matukio yaliyoweza kuthibitishwa ya uvunjifu wa Sheria, Kanuni na Miongozo iliyotolewa na **WRRB** na Taasisi nyingine za Serikali (**Bodi za Mazao**, **Mamlaka za Serikali Kuu/Mitaa**).

Vigezo tajwa hapo juu vilipangwa kwa kutumia mbinu/kipimo kwa mtindo wa *Likert Scale* kwa nambari 0,1,2,3 na 4*;* ambapo jinsi inavyokaribia 4 ndivyo ilivyo chanya katika utendaji na jinsi inavyokaribia 0 inakuwa hasi kwa utendaji. Ufunguo wa alama ni **Hafai Kabisa** (Alama 0), **Utendaji Dhaifu** (Alama 1), **Utendaji wa Kati** (Alama 2), **Utendaji Unaoridhisha** (Alama 3), **Utendaji Uliotukuka** (Alama 4).

Kwa mujibu wa kipimo hicho, kama inavyoonekana *Jedwali Na.3.3* kampuni zilizoongoza ni kama ifuatavyo:

#### 8.3.3.1. Kampuni zilizoongoza kwa ufanisi

i. **Ace Global Depository (T) Limited** iliongoza kwa ufanisi na kushika alama ya kwanza kwa kupata jumla ya **alama 4.00. Kampuni hii ilikuwa inaendesha ghala la** Tanecu Limited – Newala **lilipo Newala mkoani Mtwara chini ya Chama Kikuu cha TANECU Ltd**

ii. **Pisah Limited** ilishika nafasi ya pili **kwa kupata alama 3.75.** Kampuni hii ilikuwa inaendesha ghala la **Rufiji DC** lilipo wilayani Rufiji mkoa wa Pwani chini ya Chama Kikuu **CORECU Ltd.**

iii. **Pugna Agrifood Tanzania Ltd** ilishika nafasi ya tatu kwa kupata **alama 3.75;** Kampuni hii ilikuwa ikiendesha ghala la **Juma Ally Ngwaya – Bungu** lililopo wilaya ya Kibiti mkoa wa Pwani chini ya Chama Kikuu **CORECU Ltd**.

#### 8.3.3.2. Kampuni zilizokuwa na utendaji hafifu (chini ya alama 2.0)

i. **Mufena Company Limited** ilikuwa moja ya kampuni za mwisho yenye utendaji dhaifu ilipata **alama 1.75;** Kampuni hii ilikuwa inaendesha ghala la **Cashewnut Company (2005) Limited** lilipo Mtwara Mjini mkoani Mtwara chini ya Chama Kikuu cha **MAMCU Ltd.**

ii. **Vika General Company Limited** ilikuwa moja ya kampuni za mwisho yenye utendaji dhaifu ilipata **alama 1.75;** Kampuni hii ilikuwa inaendesha ghala la **Remigio V. Naga.** lilipo Masasi mkoani Mtwara chini ya Chama Kikuu cha **MAMCU Ltd.**

iii. **Mtambaswala Company Limited** ilikuwa moja ya kampuni za mwisho yenye utendaji dhaifu ilipata **alama 1.75;** Kampuni hii ilikuwa inaendesha ghala la **Ali Mohamed Salim (Millenium)** lilipo Masasi mkoani Mtwara chini ya Chama Kikuu cha **MAMCU Ltd.**

**Jedwali Na.17 Udarajishaji wa Utendaji wa Waendesha Ghala Msimu wa**

***Korosho Mwaka 2024/2025***

| N | Kampuni ya Mwendesha Ghala | Alama kati ya 4 |
|---|---|---|
| 1 | Ace Global Depository (T) Limited | 4.00 |
| 2 | Pisah Limited | 3.75 |
| 3 | Pugna Agrifood Tanzania Ltd | 3.75 |
| 4 | H & E Moonrich Comapny Limited | 3.63 |
| 5 | Nampachila Business Company Limited | 3.63 |
| 6 | Bojomosa Agriventure Company Limited | 3.50 |
| 7 | Ahn & Raka Company Ltd | 3.50 |
| 8 | Bin Swalehe General Dealers Ltd | 3.50 |
| 9 | Ruangwa Warehousing Company Ltd | 3.50 |
| 10 | Dreams On Development Company Limited | 3.46 |
| 11 | Zuma General Trading Company Limited | 3.42 |
| 12 | Mkaba General Traders Co.Limited | 3.38 |
| 13 | Demuton Tanzania Ltd | 3.38 |
| 14 | Saesh Business Company Limited | 3.25 |
| 15 | Mandiwa Agro Products Limited | 3.25 |
| 16 | The Prominence Global Traders And Co Ltd | 3.13 |
| 17 | D&B Agribusiness Co.Ltd | 3.13 |
| 18 | Krenk Agro (T) Ltd | 3.13 |
| 19 | Stecuria Investment Company Limited | 3.00 |
| 20 | Sb Logistics & Company Limited | 3.00 |
| 21 | Makita Agrifood Limited | 3.00 |
| 22 | Tanyusa Company Ltd | 2.94 |
| 23 | Lenzaq Holdings Limited | 2.88 |
| 24 | Mikat Agribusiness Ltd | 2.88 |
| 25 | Perfect Cashew Kernel Ltd | 2.88 |
| 26 | Mafia Cashewnut & Coconut Cooperative Society | 2.88 |
| 27 | Hawa Agri (T) Limited | 2.75 |
| 28 | Cropstan Investment Limited | 2.75 |
| 29 | Tamcu Group Of Companies Limited | 2.63 |
| 30 | Liwale Tabasamu Company Limited | 2.63 |
| 31 | Kumahanda General Supply | 2.50 |
| 32 | Sumajkt Logistic Company Limited | 2.50 |
| 33 | Twenyuka Company Limited | 2.38 |
| 34 | Geju Investment And General Supply Company Limited | 2.13 |
| 35 | Miki General Traders Company Ltd | 2.00 |
| 36 | Zuboma General Supplies | 2.00 |
| 37 | Mufena Company Limited | 1.75 |
| 38 | Mtambaswala Company Limited | 1.75 |
| 39 | Vika General Company Limited | 1.75 |
| | | |
| | **Wastani** | **3.00** |

**8.4. Mipango kwa msimu wa 2025/2026**

Kama ilivyoelezwa awali, Bodi ya Usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni taasisi ya umma chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Stakabadhi za Ghala Na. 10 ya mwaka 2005 na marekebisho yake kupitia Kifungu cha 4, Sura 339 R.E. 2016. Majukumu yake yameainishwa katika Kifungu cha 5 (a-j), ikiwa ni pamoja na kutoa leseni kwa waendesha ghala, mameneja dhamana na wakaguzi wa ghala; kuchapisha na kuidhinisha vitabu vya stakabadhi za ghala; kusajili na kuhifadhi taarifa za wadau muhimu wa mfumo; pamoja na kuiwakilisha nchi katika masuala ya kitaifa na kimataifa yanayohusu Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Pia, WRRB hutekeleza majukumu mengine kwa mujibu wa maelekezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara.

Katika kuelekea msimu wa 2025/2026, WRRB imepanga kutekeleza yafuatayo kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wa mfumo na kuongeza tija katika sekta ya kilimo:

i. Kuendelea kutoa leseni kwa waendesha ghala, wakaguzi wa ghala, na mameneja dhamana kwa kuzingatia viwango na masharti yaliyowekwa kisheria;
ii. Kushiriki maandalizi ya mwongozo kwa kuweka vipengele maalum vinavyohusu usimamizi wa ghala kuu za korosho;
iii. Kufanya ukaguzi wa ghala ikiwahusisha kabla ya msimu, wakati wa msimu, na takwimu baada ya kufungwa kwa msimu ili kuhakikisha ghala yanazingatia viwango vya ubora na usalama;
iv. Kusimamia matumizi ya kanzidata ya mfumo inayohusisha na ukusanyaji wa takwimu na za bidhaa zinazopokelewa na kutolewa ghalani;
v. Kutoa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa mfumo wakiwemo waendesha ghala, wanunuzi, vyama vya wakulima na wadau wengine wenye maslahi katika Mfumo;
vi. Kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya ubora kutoka kwa taasisi nyingine za udhibiti kama vile Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

## AGENDA NA. 9: TAARIFA KUTOKA SOKO LA BIDHAA TANZANIA (TMX)

## 9.0 TAARIFA KUTOKA SOKO LA BIDHAA TANZANIA (TMX)

### 9.1 Utangulizi

Kufuatia maelekezo ya Serikali kupitia Wizara ya Kilimo ya Kuuza zao la Korosho kupitia Mfumo wa Soko la Bidhaa Tanzania, Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na Soko la Bidhaa Tanzania, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala, Tume ya Maendeleo ya Ushirika pamoja na Wadau wengine imesimamia na kuendesha shughuli za minada kupitia mfumo wa mauzo wa kielektroniki wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX); kwa lengo la kuweka mazingira ya uwazi na ushindani katika biashara ya zao la Korosho ili kuongeza tija kwa wakulima kwa kuongeza kipato kutokana na zao hili kama ilivyo adhima ya Serikali. Katika Msimu wa 2024/25, jumla ya Mikoa Saba (7) inayozalisha zao la Korosho imeuza kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghala na Soko la Bidhaa Tanzania, mikoa hiyo ni pamoja na Mtwara, Lindi, Ruvuma, Pwani, Morogoro Singida pamoja na Tanga ambapo jumla ya **kilo 409,039,713** zenye thamani ya shilingi za kitanzania **1,468,905,696,522.72** ziliuzwa.

### 9.2 Maandalizi kuhusu mauzo ya korosho

Maandalizi ya kuuza Korosho kupitai mfumo wa Soko la Bidhaa yalifanyika vizuri kwa kushirikiana na wadau wote ikiwa ni pamoja na elimu kutolewa kwa Wanunuzi jinsi ya kununua, Vyama Vikuu vya Ushirika pamoja na wadau wengine. Pia kuwa na vifaa vya kuwezesha wakulima kufuatilia minada (TV & Projector) kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya Ushirika, uwepo wa Ofisi ya Soko la Bidhaa katika ofisi za Bodi ya Korosho ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kutoka Soko la Bidhaa

### 9.3 Uendeshwaji wa minada

Utaratibu na uendeshwaji wa Minada ulifanyika kwa ushirikiano mkubwa baina ya wadau husika wakiwemo Soko la Bidhaa Tanzania, Bodi ya Korosho pamoja na Vyama Vikuu vya Ushirika. Ushirikiano huu uliwezesha pamoja na mambo mengine:

i. Uandaaji wa kabrasha la Mauzo kwa wakati na kwa ufanisi;
ii. Kukubaliana juu ya bei ya kuanzia (Kinga bei);
iii. Utatuzi wa changamoto zilizokuwa zinajitokeza wakati na baada ya mnada kufanyika;
iv. Uwasilishwaji wa taarifa za ridhio la kuuza/ kutokuuza kwa wakati;

### 9.4 Mauzo ya korosho kupitia Soko la Bidhaa Tanzania

Katika msimu wa mauzo ya korosho 2024/25, jumla ya kilo 409,039,713 ziliuzwa kupitia mfumo wa Soko la Bidhaa Tanzania. Mchanganuo wa mauzo haya ni kama ifuatavyo:

**Mchanganuo wa mauzo kwa Mkoa**

| Na | Mkoa | Kilo | Thamani (Tzs) |
|---|---|---|---|
| 1 | Mtwara | 240,843,386 | 873,548,505,950.84 |
| 2 | Lindi | 115,680,505 | 417,013,825,817.20 |
| 3 | Ruvuma | 31,608,038 | 107,582,102,395.72 |
| 4 | Pwani | 19,950,228 | 67,788,134,058.32 |
| 5 | Morogoro | 370,601 | 1,153,786,930.44 |
| 6 | Singida | 172,073 | 577,650,930.12 |
| 7 | Tanga | 414,882 | 1,241,690,440 |
| | **JUMLA** | **409,039,713** | **1,468,905,696,522.72** |

**Mchanganuo wa Mauzo kwa Chama Kikuu cha Ushirika**

| Na. | Chama Kikuu cha Ushirika | Mkoa | Kilo | Thamani (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | TANECU LTD | Mtwara | 124,072,441 | 454,854,956,260.04 |
| 2 | MAMCU LTD | Mtwara | 116,770,945 | 418,693,549,690.80 |
| 3 | RUNALI LTD | Lindi | 73,826,620 | 266,818,106,477.80 |
| 4 | Lindi Mwambao Ltd | Lindi | 41,853,885 | 150,195,719,339.40 |
| 5 | TAMCU LTD | Ruvuma | 31,608,038 | 107,582,102,395.72 |
| 6 | CORECU LTD | Pwani | 19,950,228 | 67,788,134,058.32 |
| 7 | UKICU LTD | Morogoro | 370,601 | 1,153,786,930.44 |
| 9 | CEAMCU | Singida | 172,073 | 577,650,930.12 |
| 10 | TACACU | Tanga | 414,882 | 1,241,690,440.08 |
| | **JUMLA** | | **409,039,713** | **1,468,905,696,522.72** |

**Mchanganuo kwa Wanunuzi**

| Na | Jina la Mnunuzi | Kilo | Thamani (TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | A and V Group Ltd | 99,609 | 348,276,891.96 |
| 2 | ACORP EXPORT LIMITED | 454,969 | 1,798,660,300.36 |
| 3 | AFAGRI GLOBAL LIMITED | 728,940 | 2,743,536,663.60 |
| 4 | Afri (EA) Ltd | 795,428 | 2,845,018,636.32 |
| 5 | Africa Harmony Industries & Trade LTD | 2,007,288 | 6,920,167,724.72 |
| 6 | Afrisian Ginning Ltd | 2,165,689 | 7,519,477,267.16 |
| 7 | Afritech Greencrops Group Company Limited | 2,325,284 | 6,072,092,778.96 |
| 8 | AGRO PULSES EXPORT TANZANIA LTD | 1,572,768 | 5,537,916,705.92 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9 | Agro Valley Tanzania LTD | 2,756,167 | 10,465,846,545.48 |
| 10 | Agrolink Exports Tanzania Limited | 1,548,100 | 5,150,474,387.00 |
| 11 | AGS EAST AFRICA LTD | 3,287,664 | 12,070,910,516.16 |
| 12 | Alpha Namata company Ltd | 21,034,037 | 80,917,058,645.28 |
| 13 | ALPHAVILLAH COMPANY LIMITED | 7,700,553 | 26,936,453,286.32 |
| 14 | ANANUTS AGRO COMMODITY (TZ) LTD | 1,791,617 | 6,320,723,003.48 |
| 15 | ATMTOT COMPANY LIMITED | 2,954,913 | 10,614,226,619.72 |
| 16 | CDJKL NUTS LTD | 859,144 | 2,812,633,757.36 |
| 17 | CEDAR EXIM LIMITED | 644,755 | 2,488,649,922.20 |
| 18 | CNB BROTHER TECHNOLOGY LIMITED | 1,026,856 | 3,377,543,662.64 |
| 19 | Coastal Nuts (T) limited | 2,159,753 | 6,138,322,529.32 |
| 20 | COMAFRIQUE TRADING LIMITED | 3,385,647 | 12,561,037,851.68 |
| 21 | Dorman (Tanzania) Ltd | 19,796,669 | 77,928,847,663.36 |
| 22 | DUNAMIS AGRIC LIMITED | 16,858,658 | 61,906,667,037.52 |
| 23 | EMMPIRE COMMODITIES LIMITED | 2,747,972 | 9,266,592,975.68 |
| 24 | EQUATOR VENTURES COMPANY LTD | 185,960 | 736,510,522.40 |
| 25 | EXODUS AGRO EXPORT | 1,664,575 | 5,932,211,733.00 |
| 26 | EXPORT CONNECT TANZANIA | 4,180,908 | 14,259,538,937.52 |
| 27 | Export Trading Company | 52,998,427 | 198,071,704,499.88 |
| 28 | FARHEEM CO LIMITED | 319,925 | 962,793,717.00 |
| 29 | FI Commodities Tanzania LTD | 1,747,921 | 5,709,224,271.24 |
| 30 | GLC HOLDING LIMITED | 58,108 | 115,428,055.52 |
| 31 | GLOBAL GOLDEN GRAINS LTD | 170,584 | 519,673,920.96 |
| 32 | GOLDEN CASHEWS LIMITED | 6,956,556 | 25,089,196,940.64 |
| 33 | GOLDEN NUTS CASHEW COMPANY LIMITED | 172,094 | 455,371,875.36 |
| 34 | Harmony Agro Ltd | 1,984,924 | 6,957,681,720.56 |
| 35 | HS Impex Limited | 11,367,678 | 41,470,937,696.32 |
| 36 | INDOTECH TANZANIA LIMITED | 2,613,102 | 9,253,465,426.88 |
| 37 | ISCON COMMODITIES (T) LTD | 37,057,350 | 137,778,322,639.00 |
| 38 | Karibu Kilimo Limited | 94,746 | 362,539,884.24 |
| 39 | KASUGA GENERAL TRADERS LTD | 1,475,399 | 5,934,663,809.56 |
| 40 | KISASIKA AND COMPANY LIMITED | 61,659 | 239,634,003.96 |
| 41 | Kopac CO Ltd | 20,880,199 | 77,786,108,841.56 |
| 42 | Leyan Commodities Tanzania Ltd | 2,241,394 | 6,751,245,507.36 |
| 43 | Lion Agro Global Limited | 2,760,762 | 10,291,268,027.28 |
| 44 | LISTRAM COMMODITIES COMPANY LIMITED | 95,780 | 223,229,723.20 |
| 45 | MAKANJIRO OMPANY LIMITED | 4,802,880 | 16,390,232,177.20 |
| 46 | MAKONDE NUTS EXPOTERS LTD | 4,924,911 | 15,378,660,086.84 |
| 47 | MATEAK HOLDINGS LIMITED | 4,770,737 | 13,677,730,606.28 |
| 48 | MATRICS OVERSEAS LIMITED | 3,837,061 | 12,953,274,842.84 |
| 49 | MAYANI ENTERPRISES LTD | 239,993 | 923,118,674.92 |
| 50 | Megnacio Company Limited | 3,380,302 | 9,353,955,444.88 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 51 | Mohamed Entreprises | 3,436,037 | 12,343,149,938.28 |
| 52 | Nine Five Group Ltd | 3,743,538 | 11,356,443,674.72 |
| 53 | OSPHER INTERNATIONAL LIMITED | 5,769,975 | 20,926,618,629.00 |
| 54 | PARAMOUNT COMMODITIES LIMITED | 8,374,409 | 31,122,894,623.96 |
| 55 | Paramount Exim LTD | 538,085 | 1,602,479,247.40 |
| 56 | PH AGRO COMMODITIES LIMITED | 8,205,890 | 29,580,070,981.60 |
| 57 | PROSCOM TANZANIA COMPANY LIMITED | 11,306,821 | 40,260,693,687.24 |
| 58 | PSC AGRO IMPEX COMPANY LIMITED | 624,264 | 2,150,462,310.16 |
| 59 | R. V. Exports Ltd | 7,136,818 | 24,373,335,117.92 |
| 60 | RAA TRADING TANZANIA LIMITED | 369,683 | 1,289,757,178.52 |
| 61 | Rajan Agro Exports Ltd | 1,107,223 | 2,870,019,046.12 |
| 62 | Renatus Tanzania LTD | 4,632,140 | 16,765,450,676.60 |
| 63 | RIYA STAR COMMODITIES LIMITED | 1,690,698 | 5,836,820,735.12 |
| 64 | Robust Agro Commodities Trade International Limited | 2,682,551 | 10,790,214,968.44 |
| 65 | S R IMPEX TANZANIA LIMITED | 1,136,598 | 4,774,499,861.12 |
| 66 | Sedaco Agro Tanzania Ltd | 9,364,237 | 35,811,015,826.28 |
| 67 | SG TRADE TANZANIA LIMITED | 12,244,059 | 41,468,045,759.96 |
| 68 | Shri Salasar Export Tz Limited | 3,793,694 | 10,159,475,309.36 |
| 69 | SIMBA KOROSHO LIMITED | 1,764,552 | 7,282,975,764.88 |
| 70 | SM HOLDINGS | 3,982,058 | 15,002,413,903.52 |
| 71 | SPEED COMMODITIES COMPANY LTD | 4,786,232 | 17,828,869,384.08 |
| 72 | STAR ARISE TANZANIA LIMITED | 1,835,669 | 6,234,769,048.36 |
| 73 | T.C AGRICULTURE COMPANY LIMITED | 244,494 | 886,642,821.36 |
| 74 | TAMBULI GROUP OF CO LTD | 736,421 | 2,768,870,471.24 |
| 75 | TANDAHIMBA NEWALA COOPERATIVE UNION LIMITED | 1,058,792 | 3,159,473,820.48 |
| 76 | TANZIND INTERNATIONAL LIMITED | 49,504 | 127,192,865.76 |
| 77 | THE BLUE MOON AGRO LIMITED | 481,977 | 1,869,165,971.88 |
| 78 | THREE LEAVES COMMODITY TZ LIMITED | 15,417,817 | 56,514,043,881.48 |
| 79 | VNBP TRADING OMPANY LIMITED | 22,779,062 | 73,430,972,059.28 |
| | **JUMLA** | **409,039,73** | **1,468,905,696,522.72** |

### 9.5 Mafanikio

Msimu wa mauzo ya korosho wa 2024/25 umekuwa na mafaniko makubwa yaliyochangiwa kwa kiasi kikubwa na ushirikiano wa wadau wote katika biashara ya korosho. Mafanikio hayo ni pamoja na:

**i. Ushindani katika minada**

Kutokana na usimamizi Madhubuti katika biashara ya Korosho na kufuatia uhitaji wa Soko na matumizi ya Mfumo wa mauzo wa kielektroniki uliongeza uwazi na ushindani kwa Wanunuzi uliopelekea Wakulima kupata bei yenye tija;

**ii. Uwazi katika mauzo**

Mauzo ya Korosho kupitia mfumo wa Kielektroniki yameongeza uwazi kwa wadau wote kuanzia kwa Wauzaji, Wanunuzi na wadau wengine ambapo kila mmoja aliweza kufuatilia mubashara mwenendo wa mnada pindi ulipokuwa unafanyika. Uwazi huu ulisaidia hata katika suala la maamuzi ya kuongeza bei kwa wanunuzi na maamuzi ya kuuza kwa wakulima mara tu walipotakiwa kufanya hivo;

**iii. Upatikanaji wa taarifa**

Taarifa za bei, mauzo na mwenendo wa mauzo ya korosho ulipatikana kwa urahisi kwa kila mdau na kuwezesha kufanya maamuzi yaliyohitaji taarifa hizi;

**iv. Ongezeko La wanunuzi katika minada**

Katika msimu wa mauzo 2024/25, utaratibu wa kuuza Korosho kwa njia ya kielektroniki uliwezesha ongezeko la wanunuzi wengi walioshiriki na kununua Korosho chini Tanzania kwa kuwa mnunuzi alikuwa na uwezo wa kushiriki kununua kutokea popote hata nchi za nje.

**v. Ongezeko la Korosho zilizouzwa kupitia mfumo rasmi**

Kutokana na Usimamizi madhubuti wa Serikali kupitia taasisi zake na wadau wengine wa zao Korosho, tumeshuhudia kiasi cha Korosho zilizouzwa na kurekodiwa katika mfumo rasmi kimeongezeka maradufu na kupekelekea pia ongezeko la pato la Serikali na Wadau wengine kupitia tozo na ushuru

### 9.6 Changamoto

Pamoja na Mafanikio yaliyopatikana katika mauzo ya Korosho msimu wa 2024/25, zipo changamoto zilizobainika ambao ni pamoja na:

**i. Mtandao hafifu katika baadhi ya maeneo ya minada**

Baadhi ya vijiji vilivyoteuliwa kwa ajili ya wakulima kufuatilia minada na kufanya maamuzi ya kuuza au kutouzwa yalikuwa na changamoto ya upatikanaji wa mtandao (internet) wenye nguvu hususani katika vyama vya MAMCU;

**ii. Matumizi ya ghala moja kwa Vyama Vikuu zaidi ya kimoja**

Chama kikuu cha TANECU na MAMCU kutumia ghala moja Micronix System lililoko

Masasi kuhifadhi korosho kulileta changamoto hasa wakati wa uandaaji wa Kabrasha la Mauzo lakini pia kukua makusanyo ya TANECU na MAMCU katika ghala husika kwa kuwa taarifa katika za Mapokezi ya Korosho Ghalani kwenye kanzidata ya WRRB haiwezi kutofautisha korosho za TANECU na za MAMCU;

**iii. Utofauti wa taarifa za ubora wa korosho**

Minada iliyofanyika mwishoni mwa msimu, kulikuwepo na baadhi ya ghala ambazo ubora wa korosho ulioripotiwa katika kanzidata na kuingizwa kwenye kabrasha la Mauzo ulikuwa tofauti na hali halisi ya korosho baada ya Mnunuzi kununua na kwenda kuhakiki ubora wa korosho hizo hata kupelekea baadhi ya wanunuzi kukataa kulipia;

**iv. Upungufu wa kiasi cha korosho kwa wanunuzi**

Baadhi ya Wanunuzi walipata kiasi cha korosho pungufu na kiasi walichonunua;

## 9.7 Mapendekezo

Yafuatayo ni mapendekezo katika kuboresha mauzo ya Korosho kwa msimu ujao wa 2025/26:

i. **Suala la ubora wa korosho kabla mnada**

   Uwepo mkakati maalum wa kusimamia na kuhakikisha suala la ubora wa korosho unaowasilishwa na watunza ghala unaendana ubora halisi wa korosho hususani katika minada ya mwishoni. Ikiwezekana katika minada ya mwisho Bodi ya Korosho ifanye uhakiki wa ubora wa Korosho kabla ya kuzipeleka sokoni ili kujiridhisha;

ii. **Uhakiki wa uwepo wa korosho kabla ya mnada**

   Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho na Vyama, ifanye uhakiki wa uwepo wa uwepo wa Korosho ghala hasa kwa minada ya mwishoni mwa msimu ili kuepuka kuuza mzigo hewa;

iii. **Fidia kwa wanunuzi wanaokosa korosho baada ya kulipia**

   Wanunuzi wanaokosa Korosho ghalani walipwe fidia kama mwongozo unavyotaka hasa baada ya WRRB kuhakiki madai yako ili kulinda na kujenga Imani kwa Wanunuzi ukizingatia kuna tozo ya kufidia ukosefu wa korosho kwa Wanunuzi;

iv. **Utunzaji wa korosho za Vyama zaidi ya Chama kimoja katika ghala**

Ili kuepuka kuchanganya korosho hususani wakati wa uandaaji wa kabrasha la mauzo na taarifa za makusanyo kwa kila ghala ni vema ghala moja likatunza korosho za Chama Kikuu kimoja. Maeneo ya vijiji yanayochaguliwa kwa ajili ya wakulima kushudia minada inashauriwa yazingatie upatikanaji mzuri wa mtandao wa internet

## 9.8 Hitimisho

Ili kulinda uaminifu wa mfumo wa mauzo kupitia Soko la Bidhaa, mfumo huu unategemea zaidi kumuuzia mnunuzi taarifa ambayo ni sahihi ili afanye maamuzi ya bei kulingana na taarifa uliyompatia kwenye kabrasha la mauzo. Hivyo, wadau wote tushirikiane kuhakikisha kwamba taarifa tunayompatia mnunuzi wakati wa mauzo iandane na hali halisi ya mzigo uliopo ghalani ili kuendelea kulinda Soko la Korosho ndani nan je ya nchi, kwani wanunuzi wengi wapya wanaojitokeza kununua wanakuja na hofu ya uhafifu wa ubora na upungufu wa uzito au kukosa kabisa mzigo ghalani hasa minada ya mwishoni.

**AGENDA NA. 10: TAARIFA KUTOKA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA**

## 10.0 TAARIFA KUTOKA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA

### 10.1 Utangulizi

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania ni taasisi inayojitegemea chini ya Wizara ya Kilimo ambayo iliundwa kupitia sheria ya Vyama vya Ushirika ya Mwaka 2013. Kupitia sharia hii,Tume imepewa mamlaka ya kuhamasisha, kuthibiti na kusimamia maendeleo ya Vyama vya Ushirika nchini.

### 10.2 Majukumu ya Tume katika kusimamia mauzo ya korosho

Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika majukumu yake ya kuhamasisha, kuthibiti na kusimamia shughuli za Vyama vya Ushirika nchini na katika vyama vya Korosho Tume inafanya yafuatayo;

i. Kutoa waraka wa Usimamizi wa Biashara na masoko ya Korosho kila msimu,
ii. Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kuandaa Mwongozo wa Mauzo ya Korosho kila Mwaka.
iii. Kushirikiana na Bodi ya Korosho kuhakikisha kuwa Vyama vya Ushirika vina ratibu uingizaji na ugawaji wa Pembejeo kwa wakulima kwa wakati,
iv. Kuhakikisha kuwa Vyama vya Ushirika vinakuwa na wasafirishaji wa mazao kutoka kwenye vituo vya kukusanyia kwenda ghala kuu za minada,
v. Kuratibu na kuhakikisha kuwa Vyama vya ushirika vinakuwa na vifaa na vitendea kazi kama vile; vitabu vya Stakabadhi, Ghala, Vipima unyevu, Mizani za kidigitali zilizohakikiwa na Vifungashio
vi. Kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa mara kwa mara hususani kipindi cha msimu wa mauzo ya korosho;
vii. Kuhakikisha vyama vya Ushirika vinawalipa wakulima kwa wakati baadha ya mauzo;
viii. Kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania kuratibu mafunzo ya Ubora wa korosho kwa makarani wapimaji;
ix. Kuhamasisha na kuratibu upatikanaji na matumizi ya mizani za kidigitali pamoja mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika kielektroniki (MUVU);
x. Kuhamasisha ujenzi wa viwanda kwa ajili ya kuongezea thamani zao la korosho;
xi. Kutatua migogoro mbali mbali ambayo inaweza kujitokeza kipindi cha mauzo.

**10.3 Utekelezaji na usimamizi wa zao la korosho msimu 2024/2025**

Katika msimu 2024/2025, Tume ya Maendeleo ya Ushirika ilisimamia Vyama vya ushirika vipatazo 719 vikiwemo Vyama Vikuu vya Ushirika 9 katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma, Pwani, Tanga, Morogoro na Singida. Katika utekelezaji huo, Tume ilifanya kazi zifuatazo,

i. Kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho, Tume iliandaa mwongozo wa Mauzo ya korosho msimu 2023/2024;
ii. Tume ilitoa Waraka wa Usimamizi kwa Vyama vya Ushirika vya Korosho nchini;
iii. Tume ilifanikiwa kusimamia kikamilifu malipo ya Fedha za mauzo ya Korosho kwenda kwa wakulima;
iv. Tume ilisimamia mauzo ya korosho kupitia minada iliyakuwa inafanyika kwa uratibu wa Vyama vikuu;
v. Tume kwa kushirikiana na wadau wengine ilisimamia mauzo ya korosho kupitia soko la awali;
vi. Tume ilisimamia kikamilifu ununuzi wa Vifungashio/gunia kupitia vyama vya Ushirika;
vii. Tume iliratibu na Kusimamia upatikanaji na ugawaji wa pembejeo;

**10.4 Mafanikio yaliyofikiwa msimu 2024/2025**

i. Uzalishaji kuongezeka kwa Zaidi ya asilimia 60 (60%) ukilinganisha na msimu 2023/2024;
ii. Malipo ya fedha za mauzo kufanyika kutoka UNIONs moja kwa moja kwenda mkulima;
iii. Bei ya korosho kuongezeka kutoka bei ya juu ya **sh.2,190/=** kwa kilo mwaka 2023/2024 mpaka **sh.4,195/=** kwa kilo mwaka 2024/2025;
iv. Ukarabati na ujenzi wa maghala kutokana mapato ya ushuru kwenye AMCOS;
v. Kiwanda cha kubangua korosho cha TANECU LTD chenye uwezo wa kubangua **kilo 3,500,000 kuzinduliwa** rasmi ambako kimeweza kubanguo korosho kwa kuanzia **kilo 365,000** msimu 2024/2025;

vi. Baadhi ya Vyama vya Ushirika kununua malori kwa ajili ya kusafirisha korosho kutoka AMCOS kwenda ghala kuu; mfano, **RUNALI ltd** ilikuwa na lori moja sasa wamenunua mengi saba na sasa wana **lori 8**, **Luatala AMCOs** Lori 1 na **Nanyumbu AMCOS** Lori 1 na **MAMCU LTD** wanatarajia kununua **malori 10** kabla kuanzia kwa msimu ujao wa korosho, hii ni kuhakikisha changamoto ya usafirishaji wa korosho inapungua au kuisha kabisa;

vii. Usambazaji na matumizi ya mizani za kidigitali umefikia asilimia 98 ambako jumla ya **mizani 2,321** zilisambazwa kwenye vituo vya kupimia korosho kwenye kila AMCOS katika mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara na Ruvuma.

**10.5 Changamoto zilizojitokeza msimu 2024/2025**

Katika utekelezaji wa kazi za usimamizi kipindi cha mauzo ya korosho msimu uliyopita, kuna baadhi ya changamoto zilijitokeza kama vile;

i. Dosari kubwa katika taarifa za akaunti za wakulima ambazo zilikuwa zikiwasilishwa ikiwa ni pamoja na akaunti hizo kuwa zimelala, kutofautiana kwa majina ya akaunti, nk;

ii. Ucheleweshaji wa malipo ya fedha za korosho za wakulima kwa baadhi ya Vyama Vikuu vya Ushirika;

iii. Baadhi ya wanunuzi kuchelewa kutoa mizigo yao ghala kuu na kusababisha ghala kujaa;

iv. Uhaba wa vyombo vya usafiri kama vile malori kipindi cha msimu hususani kutoa korosho AMCOS kwenda ghala kuu;

v. Baadhi ya kampuni zilizokuwa zinanunua korosho kupitia soko la awali kuchelewa kufanya malipo kwa wakati;

vi. Upungufu wa vifungashio kutokana na uzalishaji kuwa mkubwa kulinganisha na matarajio;

vii. Baadhi ya AMCOS kutotumia mizani za kidigitali kwa ufanisi.

**10.6 Mikakati na maandalizi ya msimu 2025/2026**

Katika kuelekea msimu 2025/2026 Tume imejiwekea mikakati ifuatayo;

i. Kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho kuandaa na miongozo ya mauzo na ubora wa korosho kwa msimu 2025/2026;

ii. Tume itatoa waraka wa Usimamizi wa biashara ya Korosho kwa Vyama vya Ushirika vyote vinavyojishughulisha na zao la Korosho;

iii. Tume imejipanga kusimamia kikamilifu Mauzo na Malipo ya fedha za Korosho kwa wakulima kwa kuhakikisha Maafisa Ushirika na Vyama Vikuu vya Ushirika kwenye vituo vya kuchakata malipo (payment centers);

iv. Kuhamasisha Vyama Vikuu vya Ushirika kujenga viwanda vya kubangua korosho ambako kwa sasa TANECU Ltd wataendelea na upanuzi wa kiwanda chao kufikia uwezo wa **kubangua Kilo 7,000,000** kutoka **kilo 3,500,000** yaani Newala kiwanda cha sasa kina uwezo wa kubangua kilo 3,500,000 na upanuzi utafanyikia Tandahimba ujenzi kiwanda chenye uwezo kubangua kilo 3,500,00;

v. Kuendelea kuhamasisha wakulima kukausha korosho na kuzipanga kwenye madalaja stakihi ili kuendelea kulinda ubora wa korosho;

vi. Kusimamia mikutano Mkuu ya Mwaka kwa ajili ya kupitisha na kuidhinisha bajeti za chama ikiwa ni pamoja na gharama za msimu wa korosho;

vii. Kwa kushirikia na Bodi ya Korosho na Vyama vikuu vya Ushirika kuhakikisha upatikanaji na ugawaji wa pembejeo za korosho kwa wakulima;

viii. Kuhakikisha kuwa vyama vinakarabati maghala na ujenzi wa ghala;

ix. Kusimamia upatikanaji wa vifungashio vya kutosha na kwa wakati ambako tayari Chama cha Mradi wa Pamoja wa UNIONs za Korosho (KCJE) kimeagiza **gunia 18,000,000** ambazo zinatarajiwa kupokelewa na kusambazwa kabla ya mwezi julai,2025;

x. Kuhakikisha kuwa Vyama vinaingia mikataba na waendesha ghala;

xi. Kuhakikisha vyama vinatangaza zabuni kwa wasafirishaji wa korosho kutoka kwa ghala za AMCOS kwenda ghala kuu;

xii. Kushirikiana na wadau wa fedha na mitandao ya simu kutoa elimu ya fedha na matumizi ya taarifa za akaunti za benki au simu.

xiii. Kuhamasisha matumizi ya mizani za kidigitali kwa ufanisi kupitia Maafisa Ushirika kila wilaya kuhakikisha makarani wanatumia mizani za kidigitali kupima korosho za wakulima.

**AGENDA NA. 11: MENGINEYO**

# AGENDA YA 12 KUFUNGA KIKAO

